epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Julai 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581727
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 21
**ETO'O AKALIWA KOONI CAMEROON**

UKURASA WA 4
**Wanajamii** wavamia na kugawana mali za mkandarasi aliyekimbia madeni, ashalipwa asilimia 90

UKURASA WA 5
**Volcano** yafumuka, wenyeji wageuza tope la kuchezea, RC atahadharisha



UKURASA WA 9
**MIKOPO YA 10%**
**Vikundi** vyashtakiwa kutorejesha mikopo kutoka halmashauri



# Jaji Mkuu aanika 'uchafu' mawakili

• **Ataja** kuna mambo ya aibu yanayofanywa na baadhi yao... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 22
**BARCELONA KUMUUZA KOUNDE ARSENAL**

BARCELONA wanafikiria kumuuza Jules Kounde huku klabu ya Arsenal...



## Vigingi viwili vya mrithi wa Kidata TRA



UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan na mgeni wake, Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi wakimsikiliza Mwenyekiti wa Umoja wa Wadau wa Kahawa wa Sekta Binafsi katika nchi 11 barani Afrika, Amir Esmail (kushoto), kabla ya kufungua Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: IKULU**

# Nyusi: Afrika tujitegemee, wakubwa hawatufai tena

• **Samia** asema hoja za wafanyabiashara ziko 'jikoni'... *Ukurasa 2*

**MICHEZO** **DIARRA, MUSTAFA WABAKIA TANZANIA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhi zawadi ya picha kwa Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu wa Jimbo Katoliki Lindi, Mhashamu Wolfgang Pisa, alipowasilisha salamu za pongezi kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kufuatia kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza hilo, kwenye makazi yake, Mtanda, mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**

# 'Uchafu' wa mawakili

**Na Grace Gurisha**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma amesema ni aibu baadhi ya mawakili kutolipa kodi ya pango ya ofisi zao na wengine kukimbia na fedha za wateja wao baada ya shamba kuuzwa na kupokea malipo hayo.

Amesema mahakama haiwezi kufumbia macho mawakili ambao watakiuka maadili ya kazi zao, akibainisha kuwa wamepata malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu mienendo ya baadhi ya mawakaili wakati wakifanya majukumu yao ya kazi.

Prof. Juma alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akiwapokea na kuwakubali mawakili 555, akiwataka wafanye kazi kutokana na kiapo walichokiapa mbele yake kuhusiana na maadili katika taaluma yao.

Alisema ni jukumu la mahakama kusimamia maadili na wamekuwa wanapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, hivyo Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kijitahidi kusimamia maadili ya mawakili bila kuingiliwa na watu wengine.

"Ni jukumu la mahakama kusimamia maadili, mfano malalamiko tunayoyapokea mengi mimi, Jaji Kiongozi na wengine ni ya utovu wa maadili, hatuwezi kuyafumbia macho, lazima hatua zichukuliwe," alionya.

Jaji Mkuu alisema wananchi (wateja) wanalalamika mawakili kutokurudishia nyaraka halisi pale wanapobadilisha wakili mwingine, akisema jambo hilo ni utovu wa nidhamu kwa kwua ikitokea hali hiyo ni lazima nyaraka hizo zirudi kwa mteja.

"Changamoto hizi za maadili zinatakiwa zishughulikiwe na TLS wenyewe bila kuingiliwa na ndiyo maana mawakili 100 wa kwanza waliofika mbele yangu niliwauliza 'je! mnafahamu kanuni na kifungu kinachohusiana na maadili?'

"Ni kifungu kinachoiwezesha TLS katika maadili kwa sababu kila chama kinapaswa kusimama katika maadili. Na kwa bahati nzuri mjiunge katika vyama vya kanda zinazotakiwa kuwasilisha taarifa za maadili," aliagiza.

Jaji Mkuu alisema malalamiko mengine kutoka kwa wanachi ni mikataba wa mauziano ya mashamba; wakili akipata kiasi cha malipo anakimbia na wengine hawataki kulipa pango la nyumba (ofisi) zao hadi wamikiliki wamekwenda kulalamika. Ni aibu na ni utovu wa nidhamu.

"Wengine wanapeleka taarifa mahakamani kuwa wadaiwa wamekubaliana kulipana nje ya mahakama bila wahusika kujua. Wengine wanachukua fedha za wateja hawaonekani mahakamani hadi kesi inafutwa," alisema

Jaji Mkuu pia aliwataka mawakili hao wasimamie maadili kwa sababu wananchi wanawategemea katika kupeleka malalamiko yao, vinginevyo heshima ya mahakama itashuka.

# Nyusi: Afrika tujitegemee, wakubwa hawatufai tena

**Na Waandishi Wetu**

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, amesema vita vilivyotikisa mataifa mbalimbali duniani pamoja na mlipuko wa UVIKO-19 viwe ni funzo kwa nchi za Tanzania na Msumbiji kutengeneza vitu vyao wenyewe badala ya kuendelea kutegemea kutoka nchi nyingine.

Nyusi alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), yanayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere maarufu, Sabasaba.

Alitoa mfano katika vita hivyo vilivyotokea baadhi ya nchi duniani kuwa pamoja na kutokea katika mataifa ya mbali, lakini Tanzania na Msumbiji ni miongoni mwa zilizoathirika.

"Jambo jingine kuhusiana na kuyumba kwa masoko kunakosababishwa na vita huko Ulaya na Mashariki ya Kati ambako vinachelewesha kuondoa hatari ya kupanda kwa bei ya bidhaa za nishati zinazosababisha mfumuko wa bei na gharama kubwa za ufadhili na kuathiri akaunti za umma na huduma za benki katika nchi nyingi hasa Jangwa la Sahara, vinatufundisha tutengeneze vitu kutoka kwetu," alisema Nyusi.

"Tunaona hata watu wetu wanakosa hili wanakosa lile, kwa hiyo japo tunaona kama viko mbali, lakini vinatusumbua, mfano wanachukua madini yetu wanakwenda kutengeneza huko sasa kama hawatengenezi kutokana na hicho kinachoendelea huko sisi tunaathirika, kwa hiyo pamoja na kwamba tuna matatizo, yanaongezeka zaidi, kwa hiyo ni lazima tujifunze sasa vitu vyetu tuanze kuvifanya huku kwenye nchi zetu," alisema Nyusi.

Alisema Tanzania na Msumbiji wamejipanga na kushirikiana zaidi kuboresha mazingira ya biashara ikiwamo kuharakisha ukuaji wa uchumi.

"Tunataka kushirikiana katika eneo la sekta ya viwanda, usafiri na huduma zinazojikita katika miji mikubwa pamoja na bidhaa za walaji, utumiaji na uchakataji wa pamoja wa bidhaa ambazo ni za kawaida kwa pande zote mbili ikiwamo korosho, katani na mkongo ili kuongeza kiwango cha ukuaji wa kibiashara. Haya yatashawishi kuundwa kwa sekta ya viwanda na kuchochea utafiti wa kisayansi utakaoleta kipato kwa familia na maendeleo ya nchi.

Alisema mara nyingi wakulima katika nchi hizo wanalima korosho halafu wanauza kwa bei ndogo, lakini zikitoka nje ya nchi hizo inauzwa bei kubwa yenye utofauti.

Aliwaalika wawekezaji kutoka Tanzania kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo katika nchi ya Msumbiji kwenda kuwekeza.

"Ndugu zangu nasema hivi kwa sababu Msumbiji mtu yeyote anaweza kuwekeza, kwa hiyo kama una fedha zako, chagua ndugu yako wa Msumbiji uje uwekeze, hata kama una lima zao fulani kwa ukubwa zaidi una soko lako kwetu njoo uwekeze, msijifunge Tanzania tu," alisema Nyusi.

Kadhalika, alisema nchi hiyo ina sekta zake za kimkakati hususani katika kilimo, nishati, miundombinu, viwanda, madini, utalii, kwa sababu nchi yetu iko karibu sana na Tanzania, tupo tayari kukaribisha mipango ya uwekezaji yenye tija kutoka Tanzania katika sekta hizo za kimkakati.

Alisema Uchumi wa Tanzania ambao unategemea sana madini, utalii, madini kilimo na viwanda unatarajiwa kukua kwa kasi zaidi mwaka huu kuliko mwaka jana kwa kufikia asilimia 5.4 kutoka 5.1 za mwaka jana.

Alisema kuna haja ya nchi hizo mbili kuendelea kuonyesha fursa zao za kiuchumi na bidhaa zao ili kuchochea biashara zaidi na kuhamasisha uwekezaji zaidi ili kuchochea uchumi na maendeleo ya usalama wa chakula, ushindani kati ya kampuni ndogo ndogo na uzalishaji mali, kukuza ajira ili kufikia ustawi wa watu kwenye nchi hizo.

### ATANGAZA KUNG`ATUKA

Nyusi alitumia hadhara hiyo kutangaza kwamba hatagombea tena urais wa nchi hiyo na ataheshimu Katiba.

"Nikipewa ruhusa na Rais Samia, dada yangu, ningependa kuwataarifu kuwa nchi yangu ya Msumbiji, itakuwa na uchaguzi mkuu Oktoba 9, mwaka huu, kwa utii wa dhati wa Katiba niliyoiapa kuilinda na kuiheshimu, sitagombea tena urais. Kama Mwalimu Nyerere (Rais wa kwanza Tanzania), nitang`atuka, nawashukuru wananchi wangu kwa kipindi chote hiki walichonipa nafasi kuwaongoza," alisema Nyusi.

### SAMIA APONGEZA

Rais Samia alimpongeza Rais Nyusi kwa kukubali kuwa mgeni rasmi kwenye maonesho na kwamba ni nyenzo katika kuchochea maendeleo ya kibiashara na ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi.

Alisema serikali itaendelea kuifanya Tanzania kuwa mahali sahihi na salama kwa uwekezaji na kutoa wito kwa Watanzania kutembelea na kushiriki maonesho hayo makubwa na kutumia vizuri programu zinazoandaliwa katika kupata wadau wa biashara na uwekekezaji.

Alipongeza kampuni 11 ambazo zimeanza kutumia fursa hiyo muhimu kwa kusafirisha bidhaa za kahawa, katani, viungo, karanga na tumbaku kwenda nchi mbalimbali za Afrika ikiwamo Algeria, Misri, Ghana na Morocco.

Alisema serikali itaendelea kufanya kila linalowezekana kusikiliza na kutatua changamoto za wafanyabiashara nchini.

Mmoja wa wafanyabiashara na Mwenyekiti wa Umoja wa Wadau wa Kahawa wa Sekta Binafsi katika nchi 11 barani Afrika, Amir Esmail, alisema kwa sasa wanafurahia mazingira ya biashara yaliyowekwa na serikali.

"Biashara kwa sasa ni nzuri sana na nimemshukuru Rais Samia kwa kufungua nchi pamoja na maandalizi mazuri ya mabanda kwenye maonesho ya mwaka huu, haijawahi kutokea mabanda kupendeza zaidi kama ilivyo mwaka huu, tunashukuru na tunapongeza sana," alisema Nyusi.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya, Christina Mwakangale na Pilly Kigome***

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

KANDA YA MBEYA

**SHAURI LA MAOMBI YA MAREJEO NA 7482 LA MWAKA 2024**

(Kutokana na Shauri la Maobi Na 26235/2023 Mahakama ya Wilaya Mbeya. Shauri asilia Madai Na. 17/2022 Mahakama ya Wilaya Mbeya)

CMG CONSTRUCTION COMPANY LIMITED.......................... MWOMBAJI

DHIDI YA

1.HERFRID JOHN MGENI
2.MOHAMED ALLY MASHANGO t/a MASHANGO::::::::::WAJIBU MAOMBI
3.INVESTMENT COMPANY LIMITED
4.LAROY AGGREGATE LIMITED
5.CHRISTOPHER MBWILO

KWA: ~~LAROY AGGREGATE LIMITED~~ CHRISTOPHER MBWIKO
POPOTE ULIPO

**KUITWA SHAURINI**

unataarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa mahakamani binafsi au Wakili wako tarehe **17/07/2024** siku ya **Jumatano** saa **3:00 kamili asubuhi**. Ambapo shauri limepangwa kutajwa.

**ELEWA KWAMBA,** Ukikosa kufika siku hiyo, shauri litapangwa kusikilizwa bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **26/06/2024.**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

THE HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

## HABARI KITAIFA

# Vigingi viwili vya mrithi wa Kidata TRA

**Na Romana Mallya**

WACHUMI na wafanyabiashara wamezungumzia uteuzi mpya wa Yusuph Mwenda kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), wakitaja mambo mawili yanayomsubiri.

Mambo hayo ni kupanua wigo wa kodi na kubadilisha au kuimarisha dhana nzima ya usimamizi wa kodi nchini.

Usiku wa kuamkia jana, Ikulu ilitangaza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko ya uongozi katika maeneo kadhaa, akimwondoa Alphayo Kidata katika nafasi ya Kamishna Mkuu wa TRA na kumteua kuwa Mshauri wa Rais Ofisi ya Rais, Ikulu.

Nafasi iliyoachwa wazi na Kidata TRA imechukuliwa na Mwenda, aliyekuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA).

Mabadiliko hayo yamefanyika ikiwa imepita wiki moja tangu kuitishwe mgomo wa wafanyabiashara katika mikoa mbalimbali nchini, wakilalamikia kuwapo utitiri wa kodi unaotozwa na TRA.

Vilevile, ni malalamiko yaliyofanywa siku chache baada ya mabalozi 10 wanaowakilisha nchi zao Tanzania, kuwasilisha malalamiko serikalini dhidi ya vikwazo vya uwekezaji wa raia wake nchini, hususani vya kikodi, wakiinyooshea kidole TRA moja kwa moja kuwa kiini cha tatizo.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hii jana kuhusu mabadiliko hayo, wachumi na wafanyabiashara walipongeza hatua hiyo, huku wakitaka kuwapo ushirikiano na utatuzi wa changamoto zinazojitokeza ili kuongeza wigo wa walipakodi nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini nchini (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema jukumu lolote ambalo mtu anakabidhiwa na Rais ni kwa ajili ya wananchi.

Hivyo, Dk. Mmari alisema linapaswa kufanywa kwa uaminifu na kusikiliza; kama ni kukusanya kodi basi iwe kwa uadilifu na kwa haki.

"Kusikiliza changamoto za wananchi, kupata ushauri, kusimamia sheria na pale ambapo sheria inaonekana kukinzana na matakwa ya maendeleo ya wananchi, uchukuliwe ushauri wa kubadilisha sheria," alisema.

Kuhusu changamoto za kimifumo na mabadiliko ya kiuongozi yanayofanywa, Dk. Mmari alisema vyote vinapaswa kutazamwa.

"Tunafahamu kuna masuala ya kimfumo na sheria. Kama sheria imeelekeza kodi inapaswa kukusanywa na kiwango ni hiki, yanapaswa kutekelezwa kisheria. Lakini sera na sheria ni kitu ambacho kinaweza kuwa na matokeo makubwa zaidi.

"Kama sheria haikidhi mahitaji ya nchi, wafanyabiashara, wazalishaji shambani na makundi mengine haitajalisha nani anaitekeleza," Dk. Mmari alisema.

Ushauri wake kwa Kamishna Mkuu mpya TRA, ni kwamba kuna kazi ya kufanya ili kupanua wigo wa kodi, kubadilisha au kuimarisha dhana nzima ya usimamizi wa kodi.

Alisema suala hilo si jukumu ambalo Kamishna Mkuu wa TRA anaweza kulifanya peke yake, bali yanahitaji mabadiliko ya kimuundo, kimfumo na kisera ambayo yako nje ya kiongozi huyo.

"Wizara ya Fedha inahusika katika kuangalia sera na sekta nyingine zinazohusika kuangalia namna ya kurasimisha shughuli mbalimbali kama za ufugaji na uvuvi, ili kila anayezalisha apate kipato na kuchangia katika kodi," alisema.

Dk, Mmari alisema Kamishna Mkuu mpya hana budi kupanua wigo ili kuongeza idadi ya walipakodi nchini na kuongeza kiasi cha kodi kinachokusanywa kulingana na Pato la Taifa ambacho kwa Tanzania kipo chini.

"Hii si kazi ambayo anaweza kuifanya Kamishna wa mapato peke yake, inahitaji pia kufanyiwa utafiti zaidi, inahitaji kuangalia kama sera inaweza kubadilishwa kidogo na kwa namna gani tunaweza kuimarisha sekta za kiuchumi hususani sekta isiyo rasmi ambayo ni kubwa ili ichangie kwenye mapato, inahitaji ushirikiano wa taasisi nyingi," alisema.

Kuhusu wafanyabiashara waliofunga maduka na changamoto zinazokabili wawekezaji wa kigeni zilizoainishwa na mabalozi, Dk. Mmari alishauri Kamishna Mkuu mpya akae na kuzichambua ili kuona kiini chake na kuzitafutia ufumbuzi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Soko Kuu la Kariakoo, Martine Mbwana, alipongeza hatua iliyochukuliwa na Rais Samia, huku akimwomba ushirikiano Kamishna Mkuu mpya ili watatue changamoto zilizopo na kufungua wigo wa watu wengi kulipa kodi.

"Leo (jana) tumekutana na Kamishna wa Forodha, kubwa tumezungumza kuhusu upokeaji mizigo bandarini na kodi za forodha kwa ujumla wake. Tunaamini Kamishna Mkuu mpya TRA atatupa ushirikiano," alisema.

Katibu wa Jumuiya hiyo, Justine Beda, alisema, "Tunatamani huyu ndugu yetu Kamishna mpya TRA afuate nyayo za mtangulizi wake aliyeondolewa, tushirikiane kutatua matatizo ya wafanyabiashara ili serikali ipate kodi yake ambayo inalipika.

"Ingekuwa bora akaangalia mchakato mzima wa malalamiko ya kodi ya wafanyabiashara na walipakodi wengine kwa kukaa na sekta husika na kupatia ufumbuzi," alisema.

### KUHUSU MWENDA

Kamishna Mkuu mpya TRA (Mwenda) aliwahi kuwa diwani wa Mikocheni na Meya wa Kinondoni (2010 hadi 2015).

Machi Mosi, 2022, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alimteua kuwa Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), akichukua nafasi ya Salum Yussuf Ali aliyetenguliwa.

Sasa anachukua nafasi ya Kidata ambaye Aprili 4,2021, Rais Samia alimteua kuwa Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo baada ya Machi 25, 2017, kuondolewa kwenye nafasi hiyo na Rais John Magufuli.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Wavamia na kugawana mali za mkandarasi aliyekimbia madeni

**Na Idda Mushi,** MVOMERO

MKUU wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli ameagiza kulipwa deni la zaidi ya Sh. milioni 46 anazodaiwa aliyekuwa mkandarasi wa ujenzi wa kisima cha maji katika Kitongoji cha Sokoine Ranchi, wilayani humo, kampuni ya Self-ink LTD.

Kampuni hiyo inadaiwa kiasi hicho cha fedha na vibarua, mamalishe na mzabuni aliyeipatia huduma.

Mkuu wa Wilaya alitoa maelekezo hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Sokoine Ranchi alikokwenda baada ya kupokea malalamiko ya wananchi.

Alisema mkandarasi huyo ambaye inadaiwa ni mtumishi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Rukwa, alishapewa asilimia 90 ya malipo ya kazi, lakini kwa sasa amesimamishwa kuendelea na ujenzi kutokana na changamoto mbalimbali.

"Jitihada mbalimbali za kumtafuta zimefanyika ili alipe madeni yake, lakini hajajitokeza, nampa siku tatu msimamizi wa mradi na kampuni yake ili kuyalipa madeni yake mara moja.

"Nia ya serikali ni kuona wananchi wanapata huduma na si karaha kutokana na huduma wanazoletewa," aliagiza Mkuu wa Wilaya.

Kiongozi huyo aliwataka wananchi kurudisha mali za mkandarasi huyo walizochukua, vikiwamo vya mradi pamoja na gari aina ya Toyota Nissan lenye namba za usajili T 471 AMK.

"Hata kama mnadai, hamtakiwi kujichukulia sheria mkononi, kuna vyombo mbalimbali vya kisheria na mamlaka mbalimbali kufuatilia haki zenu, lakini si kuchukua sheria mkononi," alionya Nguli.

Baadhi ya vibarua wanaomdai mkandarasi huyo, akiwamo Juma Daniel, walisema walipewa kazi ya kuchimba karo la tangi la maji kwa makubaliano ya malipo ya Sh. 290,000 lakini hadi sasa amelipwa Sh. 150,000.

Halima Seluhinga alisema aliwapangisha chumba katika nyumba ya wageni, hivyo anadai Sh. 500,000 na fremu ya duka Sh. 70,000 lakini hajalipwa huku baadhi ya vyombo vyake vimechukuliwa na wafanyakazi wa mkandarasi huyo.

"Niliamua kulizuia gari la mkandarasi hadi pale atakapoleta fedha zangu, lakini kwa maelekezo ya Mkuu wa Wilaya nitalirudisha kwa imani haki yangu itapatikana," alisema mama huyo.


**SUMAJKT AUCTION MART COMPANY LIMITED**

SUMAJKT AUCTION MART
Efficiency and Excellence..

## MARUDIO YA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana za mdaiwa kwa mujibu wa mkataba husika. Mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA**

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 01 | GERALD YOSIA AMIN / ONE ROOT TANZANIA LTD | NYUMBA / KIWANJA NA. P35451, C.T. No. DSMT 1032810 , ILIYOPO GOBA MATOSA - WILAYA YA UBUNGO , YENYE JINA LA GERALD YOSIA AMIN | 05/07/2024 SAA: 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| | | KIWANJA NA . P35449 , C.T.No DSMT 1033584 KILICHOPO GOBA MATOSA , WILAYA YA UBUNGO ,CHENYE JINA LA GERALD YOSIA AMIN | |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
2. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4. Dhamana itauzwa "kama ilivyo"

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**SUMAJKT AUCTION MART COMPANY LTD**
**S L P 1694, DAR ES SALAAM – TANZANIA**
**SIMU: 0753 063 481 / 0767 809 980**



## BISMILLAH RAHMAN RAHIM



Familia ya marehemu **DK. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea Marehemu **DK. Omar Ali Juma** itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **4 Julai, 2024** saa kumi jioni katika Msikiti wa **Ngazija**.

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.

Ndugu, Marafiki na Jamaa wote mnakaribihswa.

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. AMIN**





# Tope laporomoka Kigoma

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

TOPE linalodhaniwa volcano linaporomoka katika Bonde la Nyankara, Kitongoji cha Pamila, Kata ya Matendo Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Mkuu wa Mkoa Thobias Andengenye akiwataka wananchi kuchukua tahadhari ya kutofika katika eneo hilo.

Amesema kuwa haijulikani ardhi imemeguka kwa kiwango gani kwa kuwa tope hilo linaendelea kuporomoka, hivyo ni muhimu kuchukua tahadhari, ili kuzuia madhara yanayoweza kutokea kwa binadamu na viumbe hai vingine.

"Tahadhari zimechukuliwa ili kuzuia madhara, ila mpaka sasa hakuna madhara yoyote yaliyotokea kwa kuwa tope hilo ni la baridi na linadhaniwa kutokuwa na kemikali japo wananchi hawapaswi kwenda kwenye eneo hilo mpaka pale uchunguzi wa wataalamu juu ya tope hilo utakapokamilika," alisema Andengenye jana alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema wananchi wanapaswa kusitisha shughuli zozote za kibinadamu zinazofanywa katika bonde hilo ambazo ni kilimo na ufugaji, wakati wataalamu wakiendelea na uchunguzi kwa kuwa tayari wameshachukua sampuli na kuzipeleka maabara, ili kujua kama tope hilo lina madhara kwa binadamu na mazingira.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, viongozi na wananchi wa Kitongoji cha Pamila, walisema hali hiyo ilianza polepole lakini mwishoni mwa wiki iliyopita tope hilo liliongezeka na kufunika eneo kubwa la bonde hilo katika shamba la Musa Magagi, takribani kilomita 2.5 kutoka kwenye makazi ya wananchi.

Diwani wa Mtendo, Ilaki Ramadhan alisema alipata taarifa ya kuongezeka kwa tope kutoka kwa wananchi, naye akatoa taarifa kwa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ambayo ilifika na kuanza kuchukua hatua za kudhibiti madhara mara moja.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Pamila, Peter Edward alisema taarifa zinazonesha kuwa hali hiyo ilianzia kwenye bwawa la kufuga samaki katika eneo hilo, samaki wake wote walikufa na katikati ya bwawa hilo kuliibuka kichuguu kikubwa.

Alisema kuwa baada ya muda kichuguu hicho kiliongezek, kukawa na mchanga wenye majimaji sawa na tope zito, hivyo watu wakaanza kupata hofu kwamba huenda eneo hilo kukalipuka volcano kama inavyotokea maeneo mengine, hivyo kulazimika kutoa taarifa kwa mamlaka za serikali.

Mtaalamu wa Miamba na Jiolojia kutoka Ofisi ya Madini Mkoa wa Kigoma, David Ndosi alithibitisha kuwa uchunguzi wa awali umebaini hiyo ni volcano ya mchanga na maji (sand eruption volcano).

Alisema kuwa tope na maji hayo hayana moto tofauti na volcano nyingine zinazojulikana kwa watu wengi.

Ndosi alisema sehemu kubwa ya volcano kama hiyo inatokea katika maeneo yenye Bonde la Ufa na matetemeko kutokana na miamba kutikiswa, hivyo mchanga na chembechembe za maji zinazotengeneza tope kupanda juu kama ilivyotokea katika eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya Kigoma, Salum Kali alisema kuwa baada kupata taarifa hiyo juzi, aliongozana na kamati ya ulinzi na usalama kutembelea eneo hilo akiwa na wataalamu wa Ofisi ya Madini na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

## TAHA, Tanga kuimarisha kilimo cha viungo

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga imetia saini makubaliano na Asasi kilele inayojishughulisha na kilimo cha mboga, maua, matunda na viungo nchini (TAHA) kwa ajili ya kubadili kilimo hicho na kuwa cha kibiashara.

Makubaliano hayo yalisainiwa Julai 2, mwaka huu na watendaji wakuu wa taasisi hizo mbili, Dk. Jacqueline Mkindi wa TAHA na Dk. Fredreck Sagamiko wa Jiji la Tanga, makao makuu ya TAHA, jijini Arusha.

Makubaliano hayo yameainisha ujenzi wa ghala ambalo litatumika kuongeza thamani na kuhifadhi viungo katika jiji hilo, kwa ajili ya kusafirisha masoko ya nje.

"Lengo kuu la makubaliano yetu ni kubadilisha kilimo cha viungo kuwa cha kibiashara ili kutengeneza ajira za kinamama, vijana na wenye ulemavu katika Jiji la Tanga," Dk. Sagamiko alisema baada ya kutia saini makubaliano hayo.

Alisema wamechagua kushirikiana na TAHA kutokana na uwezo wa kitaalam na uzoefu wake katika kuendeleza kilimo cha viungo, utalaamu wa kisasa wa kuhifadhi zao hilo, kuongeza thamani na kuwaunganisha wakulima na masoko ya nje.

Alibainisha kwamba kilimo cha viungo kimekuwa kikifanyika Tanga tangu enzi za mababu, lakini hakijawahi kuwa na manufaa makubwa kwa sababu kinaendeshwa kienyeji.

Kwa kuanzia, halmashauri hiyo imetenga eneo la ekari tano kwa ajili ya ujenzi wa ghala hilo la kisasa ambalo litatumika kwa shughuli za kusindika na kuhifadhi viungo kabla ya kusafirishwa kwenda katika masoko ya nje.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi Kilele ya Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo (TAHA), Dk. Jacqueline Mkindi (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Tanga, Dk. Frederic Sagamiko, wakionyesha makabrasha baada ya kutiliana saini makubaliano ya kubadilisha kilimo cha viungo kuwa cha kibiashara jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkuu wa mkoa akemea uadui wakaguzi wa ndani

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amewataka wafanyakazi wa Halmashauri za Mkoa wa Kigoma kuondokana na kiburi kinachowafanya kuwaona wakaguzi wa ndani maadui.

Andengenye alisema hayo wakati akizungumza na madiwani na wakuu wa idara wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, wakati wa baraza maalum la kuwasilisha hoja 60 za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2022/23.

Alisema wakaguzi wa ndani ndio wanaoweza kusababisha halmashauri hizo kuondokana na hoja kutoka kwa CAG japo wafanyakazi wengi wamekuwa wakiwaona kama maadui.

"Tuondokane na kiburi na kuwaona wakaguzi wa ndani na wa nje kama si sehemu yetu, wao wamejitolea kutuelekeza na kuboresha mifumo ya fedha ya ndani, tukianza kuwaona kama maadui ndipo tunapoanza kuharibu, wao ni sehemu yetu, tukikaa nao na kushirikiana nao tutaepusha kuwa na hoja nyingi kipindi cha ukaguzi," alisema Andengenye.

Alizitaka halmashauri hizo kuwawezesha wakaguzi wa ndani kwa vifaa na ujuzi, ili kuongeza ufanisi katika kazi zao huku akiwataka wafanyakazi wengine kufanya matumizi yanayozingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha kigezo ambacho kimekuwa kikikiukwa na kusababisha hoja kutokea.

Aidha, aliagiza kuwa ifikapo Julai 31, mwaka huu halmashauri hizo ziwe zimefanyia kazi na kufunga hoja zote zilizoibuliwa na CAG za miaka ya nyuma na za mwaka wa fedha uliopita pamoja na maagizo matano ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Mwakilishi wa Ofisi ya CAG Mkoa Kigoma, Nelson Rwezaura, alisema sababu kubwa ya kuwa na hoja nyingi ni baadhi ya idara kudhani kuwa ukaguzi ni kwa ajili ya idara ya fedha pekee bila kutilia maanani kwamba, idara zinazofanya matumizi zina majibu sahihi juu ya matumizi zaidi ya idara inayofanya malipo.

Aliongeza kuwa watumishi hao wanapaswa kuachana na mtazamo hasi kuwa ukaguzi unalenga kuwaumiza na badala yake waone ukaguzi upo kama kipimo cha kazi na kuupenda, na kwamba wao wanajitahidi kudumisha mahusiano baina yao na wafanyakazi wengine ili kuwa katika muktadha mmoja kwamba lengo la ukaguzi ni kuboresha na kuleta ufanisi katika kazi.

Akiwasilisha hoja za CAG kwenye kikao hicho, Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Benedict Kiranda alisema kati ya hoja 31, hoja saba zimefungwa, 22 zipo kwenye utekelezaji na mbili hazijafanyiwa kazi kabisa, huku sehemu kubwa ya hoja hizo zikiangukia katika upungufu wa nyaraka na maelezo yasiyojitosheleza ya matumizi ya fedha na utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Jackson Mateso, alisema wamepokea maelekezo na maagizo yaliyotolewa na kwamba watayafanyia kazi kuhakikisha hoja zinafungwa, lakini wanaweka mikakati ya kuhakikisha halmashauri haizalishi hoja mpya.

Mateso alisema halmashauri hiyo kwa miaka mitatu mfululizo imepata hati safi na kwa mwaka wa fedha wa 2023/24 wamefanikiwa kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato kutoka makadirio ya kupata Sh. bilioni 2.267 na kupata bilioni 3.11 sawa na asilimia 146.

Alisema halmashauri yake itasimamia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utendaji wa halmashauri, ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa wananchi bila kuwapo ukiukwaji wa taratibu za fedha na utendaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maonesho ya biashara yawe chachu kuleta wawekezaji nchini

**JANA** Rais wa Msumbiji Filipe Nyusi, alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonesho ya Kimataifa ya Biashara (DITF), yanayofanyika jijini Dar es Salaam, Barabara ya Kilwa, wilayani Temeke.

Maonesho hayo ya 48 ni maarufu Sabasaba na hushirikisha taasisi, mashirika, wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali.

Mbali na washiriki kutoka ndani ya nchi, vile vile huvutia wafanyabiashara wa nje ya nchi ambao huja kuonyesha bidhaa zao na kutafuta biashara.

Maonesho hayo yaliyoanza Juni 28, yanatarajiwa kukamilika Julai 13 na yanafanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Mwaka huu washiriki walitarajiwa kuwa 3,846. Maonyesho hayo yanatarajiwa kutengeneza ajira za muda 11,712 na kwa mwaka jana kulikuwa na washiriki 3,500 wa ndani walikuwa 3,233, wa nje 267, nchi za nje 19, watembeleaji 300,701 na ajira za muda 11,687.

Nchi 26 zilizothibitisha kushiriki katika maonesho hayo Korea, Uturuki, India, Japan, Singapore, Syria, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Msumbiji, Indonesia, Mauritius, Oman, Misri, Iran, Pakistan, Rwanda na Comoro.

Nchi zingine ni Zambia, Ethiopia, Kongo DRC, Ghana, China, Urusi, Italia, Uganda, Kenya na Zimbabwe na nchi nyingi kati ya hizo zinakuja kuonesha teknolojia mpya za mashine mbalimbali.

Teknolojia hizo ni zile zinazohitajika na Watanzania katika kuanzisha viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, hivyo wafanyabiashara wa ndani ni fursa kubwa ya kutumia kujifunza kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, ubora wa bidhaa pamoja na kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zao.

Maonesho hayo yatakuwa na mambo mbalimbali yakiwamo ya siku maalum za nchi saba zinazoshiriki kwenye maonesho hayo, ambazo ni China, Japan, Korea, Iran, Misri, Urusi na India na kutakuwa na programu ya Sabasaba urithi wetu.

Kutakuwa na programu za mikutano ya ana kwa ana, siku za kampuni zinazojumuisha sekta mbalimbali ambazo zimeandaliwa kwa kushirikiana baina ya sekta binafsi na umma zikiwamo TIC, ZIPA, TPSF, CTI, TCCIA na ZNCC.

Lengo la siku hizo ni kuwawezesha wafanyabiashara wa kitanzania kupata fursa ya masoko ya nje.

Watanzania wote vikiwamo vikundi vya ujasiriamali, kampuni, taasisi za umma na binafsi ni fursa yao kushiriki kwenye maonesho hayo kwa kuwa ni jukwaa muhimu la kukutana na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali.

Kupitia maonesho hayo washiriki watapata maarifa ya kisasa ya uzalishaji, ufungashaji na usambazaji wa bidhaa, kupata masoko ya ndani na nje pamoja na ajira.


Maonesho ya mwaka huu yamebeba kaulimbiu isemayo "Tanzania: Mahali Sahihi pa Biashara na Uwekezaji'.

Kaulimbiu hiyo inalenga kuonesha dunia kuwa serikali iko tayari na inaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kufanya biashara na kuwekeza katika sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwamo sekta ya viwanda, kilimo, teknolojia, uwekezaji na utalii.

Maonesho hayo yatumike kutangaza bidhaa za ndani ili ziweze kupata soko la nje. Pia ni wakati wa kutumia teknolojia ya kisasa kuuza bidhaa zetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Utaratibu huu mpya kupima Ukimwi unatufaa, tufuate sote

**HADI** sasa sote tunajua, kuna juhudi zinazofanywa na serikali kuhakikisha jamii inajitambua kiafya zao.

Mtu anapojitambua afya yake inamsaidia kujua jinsi ya kuishi, ikiwamo kujipanga katika suala zima la kimaisha, akitambua hatua hizo kiafya na namna ya kuisimamia.

Pale anapojigundua ana hofu kutokana na kugundulika maambukizi ya virusi vya Ukimwi mapema, inakuwa msaada mkubwa. Zamani katika hali ya kujificha na kutaka wasitambulike, wanajamii walisafiri kutoka sehemu moja, kwenda mkoa mwingine kuchunguzwa afya zao kama ana maambukizi hayo ya virusi vya Ukimwi au la.

Kadri muda ulivyopita na kuwapo uzoefu kuhusu changamoto hiyo, ikapatiwa aina fulani ya ufumbuzi, ambayo watu wanaenda katika vituo vya afya na kupima afya zao, kisha hata anapotambulika kuwa na shida hizo, hatua na uangalizi zaidi na matibabu yanafanyika.

Wakati fulani, ukaja utaratibu wa kuwapo vifaa vya kupima mwenyewe na hata mtu akiwa nyumbani anajipatia huduma hiyo.

Ni tofauti na awali, ilikuwa lazima mtu afike katika kituo cha afya pekee, ndipo anapopatiwa vipimo hivyo.

Hayo yote kwa ujumla, ni maendeleo yanayoletwa na serikali, kupitia wadau kuhusiana na mustakabali wa kujali afya za Watanzania, kila mahali waliko, jumla yao wakiwa wastani wa milioni 612.7 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka juzi.

Hivi karibuni, umewekwa utaratibu mpya wa kitaifa wa upimaji wa virusi vya Ukimwi kwa vipimo vitatu, ili kuthibitisha kuwa mtu kama mtu ana maambukizi ya VVU, hali inayosaidia kuongeza wigo na usahihi wa upimaji wake nchini.

Kaimu Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi nchini, Dk. Ona Machangu, anasema ni sehemu ya magonjwa ya ngono.

Akatamka katika kikao kinachohusu maradhi ya homa ya ini, pia akitambulisha mwongozo mpya kitaifa kuhusu upimaji virusi vya Ukimwi nchini.

Anasema, mtu atapimwa au kujipima na anapogundulika kuwa na virusi vya Ukimwi, katika kipimo cha awali, atalazimika kupata vipimo vingine viwili vya uhakiki, kuthibitisha ugunduzi wa awali, kabla ya hatua za matibabu kuanzishwa.

Dk. Machangu anasema lengo mahususi hapo la kutumia vipimo vitatu, ni kuhakikisha wigo wa upimaji unaongezeka kwa kupima vipimo ambavyo vitaleta majibu sahihi, zaidi yanayoleta manufaa na kusaidia huduma za uchunguzi kwa watu ili waweze kushawishika kupima na kuanza dozi mara moja endapo watagundulika.

> **Tanzania tupo katika malengo ya kidunia ya 95 95 95 na kutokana na tafiti za viashiria zinaonyesha 95 ya kwanza ya upimaji. Kama nchi tupo asilimia 83 hivyo tunalengo hasa la kuhakikisha tunamfikia kila mtu na huduma za upimaji nchini.**

Pia Dk. Machangu anasema, ili kufikia lengo la kutokomeza maambukizi mapya ya Ukimwi ifikapo mwaka 2030, Wizara ya Afya inalenga kuendelea kuboresha huduma za upimaji huo, ili kuhakikisha kila mtu anafikiwa na huduma za upimaji na kujua hali yake ya kiafya.

"Tanzania tupo katika malengo ya kidunia ya 95 95 95 na kutokana na tafiti za viashiria zinaonyesha 95 ya kwanza ya upimaji. Kama nchi tupo asilimia 83 hivyo tunalengo hasa la kuhakikisha tunamfikia kila mtu na huduma za upimaji nchini," anasema.

Kauli ya mtaalamu huyo, inaenda mbali zaidi akitamka kwa kuusihi umma, kuendelea kujitokeza kupima afya zao, ili kutambua hali walizo nazo kiafya na kuanza dozi ya kupunguza makali ya VVU mara moja.

"Niwakaribishe Watanzania kufika kwenye vituo vya afya kupata huduma za upimaji pia kuna huduma za kujipima kwani ni vizuri kujua afya yako ili kufurahia maisha," anasema.

Mwakilishi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), Maria Kelly, anasema wao kama wadau wa maendeleo, wamejidhatiti kuendelea kusaidiana na serikali, kuhakikisha mpango huo wa upimaji unatekelezeka.

## MOI yapokea majeruhi 23 ajali kila siku, wengi ni wa bodaboda

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) imesema kwa mwezi inapokea majeruhi 700 wa ajali huku asilimia 60 wakiwa wamejeruhiwa kutokana na ajali za bodaboda.

Idadi hiyo ni sawa na wastani wa majeruhi 23 wa ajali kila siku.

Uongozi wa taasisi hiyo umesema ajali hizo huwapata waendesha bodoboda wenyewe, abiria au watembea kwa miguu ambao wanagongwa na bodaboda.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Lemeri Mchome, wakati akipokea msaada kutoka moja ya kampuni za jijini Dar es Salaam kwa ajili ya waathirika wa ajali za bodaboda.

"Ni lazima tuwekeze nguvu katika kuzuia ajali za bodaboda, ni muhimu elimu ya sheria na kanuni za matumizi ya barabara itolewe, uvaaji kofia ngumu na kwa umuhimu wa kubadili tabia hatarishi zinazosababisha kutokea kwa ajali," alisema.

Dk. Mchome alishukuru kwa msaada huo wa kuwajali majeruhi wanaotokana na ajali za bodaboda hospitalini huko na kueleza kuwa jitihada zaidi zinahitajika katika kuzuia ajali hizo.

Jumaa Almasi, Meneja Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka MOI, alisema baadhi ya wagonjwa wanafikishwa kwenye taasisi hiyo wakiwa hawana fedha za matibabu.

Alisema msaada wa viti mwendo viwili na ahadi ya kugharamia matibabu kwa majeruhi 15 ni mkubwa kwao kwa kuwa baadhi yao hawana uwezo.

Dk. Mchome akiwa mkoani Arusha hivi karibuni, alitoa elimu kuhusu kujikinga na magonjwa ya mifupa, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu kwa wananchi waliojitokeza katika kambi maalum ya matibabu.

"Ninaomba nitumie fursa hii kuwashauri wananchi wenzangu kwamba ni muhimu kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi, kufuata misingi ya lishe bora na kuwa na utamaduni wa kufuatilia mienenendo ya afya zetu," alisema Dk. Mchome.

Pia alitoa rai kwa wakazi wa Mkoa wa Arusha kuchangamkia fursa ya kambi hiyo kupata huduma za madaktari bingwa.

**Ninaomba nitumie fursa hii kuwashauri wananchi wenzangu kwamba ni muhimu kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi, kufuata misingi ya lishe bora na kuwa na utamaduni wa kufuatilia mienenendo ya afya zetu.**



Msanifu wa picha za rangi, Hemedi Lupatu, akichora picha ya Rais Samia Suluhu Hassan katika ukuta wa Banda la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), barabara ya Kilwa, juzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Serikali yaweka zuio uuzaji wa maeneo

**Na Julieth Mkireri, PWANI**

SERIKALI imezuia uuzaji maeneo katika Kitongoji cha Mbala, Kijiji Cha Chamakweza, Halmashauri ya Chalinze ili kutoa nafasi ya kupata mwafaka wa mmiliki halali wa eneo hilo ambalo lina mgogoro kwa zaidi ya miongo miwili kati ya wakulima na wafugaji.

Amri ya kusitisha uuzaji maeneo katika kijiji hicho imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, wakati wa ziara ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, aliyekwenda kusikiliza wananchi hao.

Kunenge alifikia kutoa amri hiyo kutokana na mgogoro huo huku kila upande ukidai ni wakazi halali wa eneo hilo na kila upande ukimtuhumu mwingine kuwa mvamizi na kuuza maeneo pasi na kufuata taratibu.

"Agizo langu hapa shughuli za kuuza maeneo zisimame yasifanyike mauziano. Hivi sasa wananchi mheshimu sheria zilizopo. Atakayebainika kuvunja sheria na kanuni, hatua zichukuliwe," aliagiza Mkuu wa Mkoa.

Pia aliwahakikishia wananchi kuimarishwa ulinzi katika kijiji hicho huku akitoa agizo la kuchukuliwa hatua dhidi ya watu wanaotuhumiwa kujichukulia sheria mkononi na kuwapiga wananchi.

Akiwa katika kitongoji hicho, Waziri Silaa alisema kuwa baada ya kusikiliza pande zote mbili za wakulima na wafugaji wa eneo la Mbala, Chamakweza na Pingo, atatuma timu ya wataalamu kutoka wizarani kwa ajili ya kuhakiki mipaka ya vijiji na kutambua wakazi halali kijijini huko.

"Nitaunda timu ya wataalamu kutoka wizarani kufanya uhakiki wa yaliyosemwa hapa, tutachukua uamuzi ambao hayataleta taharuki. Tutakapofikia mwafaka, tutatengeneza Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na hii itasaidia kutatua migogoro inayotokea," alisema Silaa.

Waziri huyo pia alielekeza viongozi wa vijiji kuzingatia Sheria ya Ardhi ambayo inatoa mamlaka ya ardhi kutolewa kwa kuzingatia taratibu zilizopo ikiwamo mikutano ya wananchi kwenye maeneo husika.

Waziri Silaa pia alisema wizara yake imegawa Mkoa wa Pwani katika mikoa miwili ili kurahisisha utatuzi wa migogoro iliyopo kwa muda mrefu.

Awali baadhi ya wananchi walioshiriki mkutano huo uliofanyika Mbala, waliwasilisha vikwazo vyao kuhusu mgogoro huo ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 20 bila kufikia mwafaka.

Mmoja wa wananchi hao, Ester Moreto, alimweleza waziri huyo kwamba wakazi wengi wa Kijiji cha Chamakweza ni wafugaji kwa kuwa kijiji hicho ni kati ya vilivyotengwa kwa ajili ya wafugaji.

Mbambike Kisanjo alisema wafugaji walihamia katika Kijiji cha Chamakweza baada ya serikali kuelekeza wahamie huko wakati wa Operesheni Vijiji Mwaka 1974 na baadaye wakulima walihamia kwa wingi kwenye eneo hilo, hivyo kusababisha kuwapo migogoro isiyoisha.

Mmoja wa wananchi aliyewakilisha wakulima, Hassan Kazimoto, alisema migogoro katika Kijiji cha Chamakweza ilianza mwaka 2016 baada ya kuwapo ongezeko la wafugaji kutoka maeneo mbalimbali waliohamia kijijini huko.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Usimamizi bora wa huduma waipa CRDB tuzo ya kimataifa

**BRUSSELS,** Ubelgiji

BENKI ya CRDB imetunukiwa Tuzo ya Ubora wa Huduma kwa mwaka 2024 na Jumuiya ya Ulaya ya Utafiti wa Ubora (ESQR) katika hafla ya utoaji tuzo iliyofanyika jijini Brussels, Ubelgiji juzi.

Tuzo hiyo imetolewa kwa kutambua jitihada za benki hiyo katika kuboresha usimamizi wa ubora katika huduma zake zote. Tuzo hizo zinafanyika kila mwaka zinatambua taasisi na mashirika ambayo yamewekeza katika huduma bora kwa wateja katika sekta mbalimbali, ikiwamo sekta ya fedha kote ulimwenguni.

Benki ya CRDB imekuwa ikiwekeza kwa kiasi kikubwa katika mifumo ya utoaji huduma bora inayojumuisha teknolojia za kisasa ili kutoa uzoefu bora katika kila hatua ya safari ya mteja.

Uongozi wa benki hiyo umeutaja ushindi huo unathibitisha namna walivyokuwa washirika wazuri kwa wateja na wadau wake.

Akizungumzia wakati wa kupokea tuzo hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Uriyo, alisema, "Mtazamo wetu kubuni njia bora za kuhudumia wateja umekuwa ndio msingi wa mafanikio yetu ya katika nyanja ya huduma kwa wateja na usimamizi wa ubora. Tuzo hii ni ushahidi wa bidii ya timu yetu katika kutoa huduma bora kwa wateja wetu."

Aliongeza kuwa tuzo hiyo inaakisi maono ya kimkakati ya benki hiyo chini ya mkakati wake mpya wa muda wa kati, unaojumuisha mipango mbalimbali ya huduma kwa wateja inayolenga kuboresha utoaji huduma.

Mipango hii imeimarisha nafasi ya Benki ya CRDB katika soko huku ikiimarisha uhusiano na wateja na ufanisi wa kiutendaji.

Akizungumza kuhusu tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kutambuliwa na ESQR ni hatua muhimu inayosisitiza dhamira ya benki katika ubora na umahiri katika shughuli zake zote.

"Juhudi za timu yetu katika uvumbuzi na mbinu zinazomjali mteja zinaendelea kututofautisha katika sekta ya benki. Tunaendelea kujizatiti katika kuinua viwango vyetu vya huduma na kutoa thamani endelevu kwa wateja na wadau wetu," alisema Nsekela.

Mbinu bunifu zilizochangia tuzo hiyo ni pamoja na utekelezaji mifumo ya kidijitali ya maoni ya wateja kama vile misimbomilia (QR Code) na mfumo wa jumbe fupi (SMS) zilizowapa wateja njia rahisi za kutoa maoni na kuwezesha benki kushughulikia kwa haraka.

Zaidi ya hayo, Benki hiyo imekuwa ikifanya tathmini za mara kwa mara za ubora wa huduma na utoaji bidhaa kuhakikisha uboreshaji endelevu na kuvuka matarajio ya wateja.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkoa wa Kigoma tarehe 20 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Siku hiyo ya uzinduzi ndiyo itakuwa siku ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari Mkoani Kigoma, Tabora na Katavi kwa siku saba hadi tarehe 26 Julai, 2024.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumamosi tarehe 20 Julai, 2024 hadi siku ya Ijumaa tarehe 26 Julai, 2024
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 27 Juni, 2024 na:

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

### UNUNUZI WA MAHINDI NA MPUNGA KWA AJILI YA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2024/2025 KUANZIA TAREHE 10 JULAI, 2024

**1.0 Utangulizi**

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza. NFRA hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Ununuzi wa nafaka kwa mwaka 2024/2025 utaanza rasmi **tarehe 10 Julai, 2024.**

**2.0 Bei ya Kununulia Nafaka**

Bei ya kununulia mahindi itakuwa kati ya shilingi 500 kwa kilo hadi shilingi 600 kwa kilo, na mpunga utanunuliwa kwa bei isiyozidi shilingi 800 kwa kilo. Bei hizi zimezingatia tathmini ya bei za soko na gharama za uzalishaji katika maeneo ambayo NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa nafaka.

**3.0 Njia za Ununuzi Zitakazotumika**

i. Kutumia vituo vya ununuzi vitakavyofunguliwa nchini kote, ambavyo muuzaji yeyote anaweza kupeleka nafaka zake kuuza;
ii. Kutumia Vikundi vya Ushirika,Wakulima na Wafanyabiashara wakubwa wa mazao ambao wameingia makubaliano maalum na NFRA.
iii. Mikataba ya kuiuzia mahindi NFRA kwa waombaji wote waliokidhi vigezo imeanza kutolewa tangu tarehe 01 Julai 2024 kupitia Ofisi za Kanda na Makao Makuu, Dodoma. Waombaji wote wanahimizwa kuwasiliana au kutembelea Ofisi za Kanda walipowasilisha maombi yao ili kupata majibu ya maombi yao na kusaini mikataba kwa wale waliokidhi vigezo.

**4.0 Vituo vya Ununuzi**

Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa ya Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa ya Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Singida), Arusha (Arusha na Manyara), Shinyanga (Mkoa wa Kigoma, Shinyanga na Tabora) na Kipawa (Morogoro na Tanga).

**5.0 Utaratibu wa Ununuzi**

Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima na Wafanyabiashara utafanyika kupitia mikataba maalumu ambayo Wakala unaratibu kwa kuzingatia maombi ambayo tayari yaliwasilishwa na Wadau mbalimbali kupitia Matangazo yaliyotolewa mwezi Machi, 2024.

**6.0 Utumiaji wa mizani ya kidigitali**

Kuanzia msimu huu wa ununuzi wa nafaka mwaka 2024/2025, NFRA itatumia mizani ya kidigitali katika vituo vyote vya ununuzi wa nafaka. Utaratibu huu utatumika katika vituo vyote vya ununuzi, kuhakikisha usahihi na uwazi katika vipimo vya nafaka zinazopokelewa. Hii itasaidia kuboresha ufanisi na kuondoa malalamiko yanayoweza kujitokeza katika upimaji.

**7.0 Utaratibu wa Malipo**

Malipo yote yatafanyika ndani ya siku 14 baada ya kukamilisha taratibu za kupokea nafaka.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vituo vya ununuzi, utaratibu wa ununuzi na bei katika vituo husika, wasiliana na Meneja wa Kanda/Vituo vya NFRA vilivyo karibu yako.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**

**04 Julai, 2024.**



# RC Kilimanjaro ataka wakuu wa idara kujibu hoja za CAG

**Na Mary Mosha,** SAME

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameagiza wakuu wa idara na vitengo wa halmashauri zote mkoani humo kutojitenga kujinasua dhidi ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Aidha, Babu amesema viongozi hao wamekuwa na tabia ya kujitoa kufanya kila kinachostahili kupambana na hoja hizo, wakidhani ni jukumu la mweka hazina na mkaguzi wa ndani pekee.

Akizungumza juzi katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa Halamshauri ya Same, kilichoketi kujadili hoja tisa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30 mwaka 2023, alisema ni lazima kujipanga kujibu hoja hizo.

"Hawa sio wenye hoja peke yao, nyie wakuu wa idara na wakuu wa vitengo hili ni jukumu lenu wote, mkiwaachia peke yao hawataweza kufanya hiyo kazi. Naomba suala hili lizingatiwe katika kumaliza au kupunguza hoja,"alisema.

Alisema kwa kufanya hivyo ni kukabiliana na hoja ambazo huletea halimashauri doa huku akiwataka kuhakikisha mkaguzi wa hesabu za serikali anapata vitendea kazi, ikiwemo mafuta ya gari kwa wakati na kwa haraka.

Aidha, Mkuu huyo wa mkoa aliipongeza halmashauri hiyo kwa kupata hati safi kwa miaka mitatu mfululizo pamoja na kupunguza hoja za mkaguzi kutoka 40 hadi kufikia hoja tisa.

"Ila mnavyanzo vingi sana vya mapato, tunaomba muendelee kuwa wabunifu na kuongeza bajeti,"alisema Babu.

Aidha, Katibu Tawala Msaidizi, Usimamizi, Ufuatiliaji na Ukaguzi Miradi wa mkoa wa Kilimanjaro, Ponceano Kilumbi alizitaka kuongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni hasa kwa mikopo ya wanawake, vijana na wa watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Yusti Mapande, aliahidi ushirikiano wa baraza pamoja na watendaji katika kumaliza hoja au kuzimaliza kabisa.

"Ila tunaomba zile hoja za kisera zibaki kwa ngazi ya mkoa ili waweze kuziandikia kwa ngazi ya wizara na kupatiwa majibu,"alisema Mapande.

# Vikundi 17 kizimbani kwa kushindwa kurejesha mikopo

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIKUNDI 17 vya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10, katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, vimeburuzwa mahakamani, baada ya kushindwa kurejesha Sh. milioni 80.9

Uamuzi wa kuwaburuza kortini wanufaika hao, ulitangazwa jana na Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri hiyo, Oscar Sabachua, wakati akiwasilisha Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani, lililoketi kujadili hoja kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, mwaka 2023.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alitoa mwezi mmoja kwa menejimenti ya halmashauri hiyo, fedha hizo ziwe zimerejeshwa, huku akiagiza kupelekewa orodha ya vikundi ambavyo vimekiuka matakwa ya sera ya utoaji wa mikopo hiyo ya asilimia nne kwa wanawake, vijana asilimia nne, na wenye ulemavu asilimia mbili.

Wakati anawasilisha taarifa hiyo, Sabachua, alisema tayari Halmashauri ya Hai imevifungulia vikundi vyote 17 kesi mahakamani kama ilivyoelekezwa na Msimamizi wa Kanuni za Mikopo za Mwaka 2019, na Marekebisho yake ya Mwaka 2021.

Sabachua alisema majibu ya menejimenti ni kuwa halmashauri imefanikiwa kukusanya Sh. milioni 11.7, kati ya kiasi kilichohojiwa, ambacho ni Sh. milioni 80.9, na kwamba kiasi kilichobaki ni Sh. milioni 69.2 ambazo halmashauri inaendelea na juhudi za ufuatiliaji wa kurejeshwa.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), katika taarifa yake ya ukaguzi ya mwaka 2022/2023, alitoa mapendekezo yake, akitaka kuboreshwa uhakiki, hasa wakati wa mapitio ya fomu za maombi za vikundi na mapendekezo ya miradi, ili kuhakikisha kuwa mikopo inatolewa kwa vikundi vyenye miradi endelevu, na marejesho hayo yanarejeshwa kwa wakati kulingana na mikopo yao kwenye mikataba.

Pendekezo jingine la CAG, lilikuwa ni kutoa notisi (ilani) ya siku 30 kwa nia ya kufungua kesi kwa waliokiuka sheria zote.

Akifafanua zaidi kuhusu uamuzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Dionis Myinga alisema:

"Tumeunda timu maalum ambayo kila siku ndani ya wiki, ndani ya mwezi, tunapita kwenye vikundi hivyo na kuhamasisha kuhakikisha kwamba wanalipa madeni yao; na pesa watakayokuwa wanaipata kutokana na shughuli zao, basi fedha ile wanailipa.

"Inapofika hatua ya kupeleka mahakamani hiyo ni hatua ya mwisho kabisa. Hata wale waliopelekwa mahakamani bado tunajaribu kuongea nao kwamba ili kesi hiyo iweze kuondolewa mahakamani, basi walipe madeni."

Kutokana na hoja hiyo ya CAG, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka, amemwagiza ofisa maendeleo ya jamii wilayani humo, kupeleka taarifa ya vikundi hivyo kila mwezi katika kamati ya fedha na mipango, ikionyesha status (taarifa) ya madeni yaliyolipwa na asisubiri kupeleka baada ya miezi mitatu.

Juni 13 mwaka 2023, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati akiwasilisha hotuba ya kuahirisha shughuli za Bunge, alitangaza uamuzi wa serikali wa kusitisha utoaji wa mikopo hiyo hadi utaratibu mwingine utakapoelekezwa.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KISUTU)*

CRIMINAL CASE NO. 14885 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

YUSUPH A. MOHAMED ................................ ACCUSED PERSON

To:
Yusuph A. Mohamed
Plot No.18, Block L, Muhoro Street, Kariak Area
Ilala Municipality
Dar Es Salaam City (0715 078 345)

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 12th day of JULY ........ 2024 at **08:00 am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 7th day of June, 2024

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name ..............................

Signature ..............................

Qualification/Relationship

Date ..............................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIGOMA
*(AT KIGOMA)*

CRIMINAL CASE NO. 14404 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

SADIKI YASINI MPENDA.......................................ACCUSED

To:
Sadiki Yasini Mpenda
Plot No. 536, Block N.
Legeza Mwendo Street,
Kigoma Municipality

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS.

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the **29** day of **JULY** 2024 .at **09:00 am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this **21** .day of .**JUNE** 2024

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**


**Served Upon Me/us:**

Name..............................

Signature..............................

Qualification/Relationship

Date..............................





# Watoto waandamana kulaani mauaji ya Asimwe

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATOTO kutoka Kanisa la International Evengelical Assemblies Of God Tanzania (IEAGT) Kambi ya Waebrania Mjini Shinyanga, wameandamana kulaani mauaji ya mtoto mwenye ualbino Asimwe Novath (2), ambaye aliuawa kisha kuondolewa baadhi ya viungo vya mwili wake mkoani Kagera.

Waliandamana juzi wakati wa kuhitimisha wiki ya watoto kanisani hapo, ikiwa na lengo ya kuwapatia mafundisho ya kiroho na kimwili katika kuimarisha malezi bora.

Akisoma risala kwa niaba ya watoto wenzake, Ibrahim Jacob, alisema hali ya ulinzi kwa watoto imekuwa haiwapi amani, kwamba wanalaani mauaji ya mtoto Asimwe na kuitaka jamii kuzidisha ulinzi kwa watoto wote.

Kadhalika, alisema pia wanapinga vitendo vyote vya ukatili ambavyo wamekuwa wakifanyiwa watoto vikiwamo vipigo, ubakaji, ulawiti, utelekezaji, lugha za matusi pamoja na kuozeshwa ndoa za utotoni na kukatishwa masomo.

Pia, waliwaomba wazazi na walezi kuwalea watoto katika njia ipasavyo ikiwamo ya kiroho, pamoja na kuwaruhusu kuhudhuria kwenye mafundisho mbalimbali ya neno la Mungu ili wapate baraka na kuwa na maadili mema.

Askofu wa IEAGT, hilo David Mabushi, aliwasihi wazazi kuwajibika kuwalinda watoto na kuacha kuwatelekeza hadi watakapofika hatua ya kujitegemea.

Alisema: "Tunapoona mauaji yanayoendelea leo siyo jambo la kawaida, mtoto Asimwe ameuawa kwa ushirikiano wa mzazi wake ambaye alipaswa kumlinda, lakini kwa tamaa ya pesa akamuuza mwanawe".

## 'Wanawake jitokezeni kugombea uchaguzi'

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Mary Chatanda amewataka wanawake na makundi maalum kujitokeza katika kugombea nafasi ya uongozi wa serikali za mitaa, ili kupata viongozi wenye sifa.

Chatanda alitoa wito huo juzi wakati wa mafunzo ya usambazaji wa matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa viongozi mbalimbali, watendaji na makundi maalumu iliyofanyika wilayani hapa chini ya uratibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Alisema wanawake na makundi maalumu wamekuwa wakijiweka kando inapofika kipindi cha uchanguzi, hivyo kusababisha kukosa viongozi wanawake ambao watawasemea katika masuala ya kitaifa.

Aidha, aliwataka viongozi kutumia matokeo ya sensa katika kufikisha maendeleo kwa wananchi hasa kwenye ujenzi wa zahanati, vituo vya afya pamoja na shuleni, kwani vingi vimekuwa vikijengwa sehemu ambazo za mwingiliano mdogo wa wananchi na kusababisha watembee umbali mrefu kutafuta huduma.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kahama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro alisema wanatumia takwimu za sensa katika kuwafikia wananchi na kuwapatia huduma za kimaendeleo, hususani wale wanaoishi pembezoni ambapo awali miradi mingi ilikuwa ikijengwa sehemu ambazo hazina wananchi na ikashindwa kuendelea.

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KISUTU)*

CRIMINAL CASE NO. 14885 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

YUSUPH A. MOHAMED ........................................ ACCUSED PERSON

To:
Yusuph A. Mohamed
Plot No.18, Block L, Muhoro Street, Kariak Area
Ilala Municipality
Dar Es Salaam City (0715 078 345)

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 12th day of JULY 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 7th day of June, 2024

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name ..............................

Signature ..............................

Qualification/Relationship

Date ..............................

## Vyama vya ushirika vyaitwa kuwekeza pembejeo

**Na Halima Ikunji,** TABORA

NAIBU Waziri wa Kilimo, David Silinde amevitaka vyama vya ushirika vilivyopo maeneo ya vijijini kuomba uwakala wa kusambaza pembejeo za kilimo, ili kurahisisha ufikishaji wake kwa wakulima waliopo maeneo ya pembezoni.

Alitoa wito huo juzi wakati akifungua maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya Fatuma Mwasa Ipuli mkoani hapa.

Alisema kutokana na vyama hivyo kufanya vizuri katika eneo hilo la usambazaji pembejeo ikiwemo kuwafikia wananchi kwa wakati, serikali inavishauri kuendelea kuomba ili kuwarahisishia wakulima.

Aidha, aliitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na wizara za kisekta na wadau wengine kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika katika sekta nyingine za kiuchumi ili kuwafikia wanachi wengi zaidi kwani asilimia 84 ya vyama hivyo vipo katika sekta ya kilimo na fedha.

Silinde aliahidi kuwa serikali kupitia wizara hiyo na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itahakikisha ushirika unaimarishwa zaidi ili Watanzania wengi wanufaike.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Meneja wa Mradi wa Pamoja wa Wakulima wa Tumbaku (TCJE), Goodluck Tairo alipongeza kazi inayofanywa na vyama vya ushirika ikiwemo kuhamasisha wakulima kuzingatia elimu ya kilimo bora chenye tija ili kuongeza uzalishaji.



Alisema elimu pamoja na usimamizi wake ni chachu kubwa ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo kila mwaka, hali inayopelekea wakulima kupata mafanikio makubwa na kuinuka kiuchumi.

Alifafanua majukumu makuu ya taasisi hiyo ni kusambaza pembejeo kwa wakulima, kusimamia masoko ya zao hilo ambapo hadi sasa kuna kampuni 11 zinazonunua tumbaku, kutoa elimu ya kilimo bora na kuunganisha wakulima.

Alisema hadi sasa una wanachama nane ambao ni vyama vya ushirika kutoka mikoa saba na vyama vya msingi 716.

## Waganga wanaopiga ramli chonganishi kufichuliwa

**Na Vitus Audax,**
SENGEREMA

WAGANGA wa jadi wilayani Sengerema mkoani Mwanza wamesema wapo tayari kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na jamii kuwaibua wenzao wanaopiga ramli chonganishi.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliowakutanisha waganga hao pamoja na Jeshi la Polisi, Mwenyekiti wa waganga wa jadi wilayani hapa, Shigela Mashimba alikiri kuwepo kwa waganga wa namna hiyo na kuahidi kushiriki kikamilifu katika kuwabaini.

"Sisi kwa umoja wetu kama waganga wa jadi tutashiriki kikamilifu kuhakikisha tunaibua waganga hawa ili wachukuliwe hatua za kisheria, kwani wamekuwa sehemu ya ukatili kwa watu wenye ualbino na makundi mengine," alisema Mashimba.

Kamishna wa Polisi Jamii (CP), Faustine Shilogile, aliwaeleza waganga hao kuwa vita ya kukomesha mauaji ya watu wenye ualbino ni wajibu wa kila mtu kukemea matukio hayo, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa jeshi hilo pale waonapoona viashiria vya matukio ya namna hiyo.

"Jeshi la Polisi tuliamua kuishirikisha jamii katika kuzuia uhalifu baada ya kubaini sisi peke yetu hatutaweza kwa sababu wananchi wapo mbali kidogo na polisi na ilipofika mwaka 2006 tuliamua kuwa karibu na jamii, hivyo tunahitaji ushirikiano wenu ili kuwahakikishieni ulinzi na usalama wenu na mali zenu," alisema Shilogile.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa alisema jeshi hilo halitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria wote watakaobainika kuhusika katika vitendo hivyo vya kihalifu.

Kadhalika, alisema jeshi hilo linaendelea kupokea taarifa fiche kutoka kwa kila mwananchi pamoja na waganga hao na kuwaahidi kutokutoa siri za watoa taarifa.

ama
ALHAMISI JULAI 4, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**MIEZI MICHACHE, MAFANIKIO 99%..**

## Mkoa Mwanza ndani ya operesheni Chanjo Kizazi kwa ushindi mkubwa





Ukurasa 14

## Wizara Mifugo, Uvuvi inavyozamia utafiti chanjo kunusuru binadamu kuambukizwa

AFYA

# Kambi Makonda ilivyomuunga mkono Samia

- Foleni alivyoiongezea madaktari; dawa Mil. 100/-
- Mama mtoto wa Mbeya asimulia yake miaka 7
- Aliyeangukiwa ukuta; asiyetibiwa tangu 2021...
- Yaacha ujumbe wake Rais, Bima Afya Kwa Wote

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

BAADHI ya wananchi waliojitokeza katika kambi maalum ya matibabu bure mkoani Arusha, wamesimulia awali walivyokata tamaa ya maisha, kwa kukosa fedha za kufanya vipimo katika vituo vya afya.

Juni 24 mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, akatangaza kuanza kambi hiyo ya matibabu ya kibingwa bure katika viwanja vya michezo vya Sheikh Amri Abeid.

Wananchi walijitokeza kwa wingi, hata kusababisha kuwapo foleni kubwa za kwenda kumuona daktari kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Vurugu zilijitokeza kutokana na umati wa watu , huku wagonjwa wakieleza walivyokaa miaka mingi nyumbani wanaugua kutokana na kukosa fedha za tiba.

Katika kambi hiyo, wapo wagonjwa waliotoka katika mikoa mingine ikiwamo Mbeya, Manyara, Kilimanjaro, Singida na Dodoma, kwa ajili ya kutaka kutibiwa.

Hapo ndipo ilipogundulika umati, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaamua kuziba pengo, akitumia Wizara ya Afya, kuelekeza dawa zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 100 katika kambi hiyo ya madaktari bingwa na wabobezi.

Pia, serikali ikaongeza safu ya madaktari 20 waliotoka Marekani wakijitolea, kuungana na kundi lingine liliongezwa kwa madaktari wa Kitanzania kuanzia Juni 25, katika kazi iliyokuwapo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

"Kipekee ninaomba tumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, hivi tunavyoongea kuna gari linakuja, lina dawa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100. Dawa hizo ambazo Rais Samia amezitoa kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ziko njiani..." akatamka Makonda.

Makonda anasema wamepatiwa vijana wa kujitolea wanaotoka Marekani wanaosomea udaktari na uuguzi, wapo zaidi ya 20, hivyo wanaendelea kuongeza nguvu ili kuhakikisha foleni inakuwa fupi.



Umati uliokusanyika katika 'Kambi ya Makonda' iliyotoa tiba za kibingwa bure, katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha. **PICHA: BEATRECE SHAYO**

### ALIYETOKA MBEYA

Joyce Mwaipopo anayeishi mkoani Mbeya, anasimulia imemlazimu kufika kambi hapo, kutokana na kukosa fedha za kumtibu mwanawe mwenye miaka saba, akisumbuliwa na matatizo ya kuoza viungo vya mwili.

Anasema, mifupa ya mtoto huyo inatoka na kusababisha harufu, hali anayoteseka nayo kwa miaka saba bila ya kupata suluhu.

Mama huyo anasimulia tangu alivyojifungua mtoto huyo, siku ya nne alianza kulia na hakujua kilichomsumbua na alipofika umri miezi saba akaanza kutambaa, akavunjika mkono.

"Madaktari walikuwa wananifokea, niwe makini na mtoto. Inawezekana eti mimi ni mlevi au sitaki kumlea mtoto au ni mzembe," anatamka mama wa mtoto huyo.

Anaendelea mtoto alivyofika hatua ya kwanza kutembea katika umri wa miezi tisa, akavunjika tena mguu na ndipo safari ya mateso ilivyoanza maishani mwake.

Joyce anasema, akapatiwa rufani kwenda Hospitali ya Rufani Mbeya, akashindwa kupata matibabu, kwa kukosa Sh. Milioni 1.7, hakuwa nazo.

"Ilishindikana, kwa sababu baba yangu aliweka mji wake bondi kwa Sh. 800,000 akapatiwa Sh. 400,000. Bado ule mji ukawa umepotea ikashindikana kupatiwa matibabu nikarudi nyumbani.

"Nilivyoona mwanangu anazidi kuteseka, nikirudi tena katika hiyo hospitali, sipati msaada naambiwa mpaka niwe na hizo (pesa)," anasimulia, huku akilia

"Nikarudi nyumbani, nikaona mguu unazidi kuoza, nikajipa moyo ngoja nirudi tena Hospitali ya Rufani Mbeya, lakini sipatiwi msaada, maana mifupa haipo kwenye nyonga, imetoka akapasuka na goti na kuanza kuoza," anafafanua.

Anasema, kila alipoenda hospitali hakupatiwa matibabu kwa kukosa fedha za malipo alizotakiwa, akarudi nyumbani viungo vya mwili wa mtoto vikizidi kuvunjika na mifupa kutoka.

Joyce anaeleza, hata alivyokuwa anahitaji msaada wa kusafishwa vidonda vya mtoto wake na hakuweza kupatiwa huduma hiyo, ilimlazimu kumchukua kukatwa nyama zilizooza.

"Bahati mbaya baba yangu ambaye alikuwa akinisaidia, akaugua, ambaye mpaka sasa hivi yupo kitandani. Giza likazidi kuwa nene. Namshukuru Mungu nilisikia hili tangazo la matibabu katika radio, nikaongea na watu wanaonipa msaada wa nguo na fedha, nikawaambia natamani ningefika huko, nasikia kuna mkombozi amejitokeza Makonda.

"Saa nane kuna 'mkaka' mmo-

INAENDELEA UK.13

AFYA

## MIEZI MICHACHE, MAFANIKIO 99%...

# Mkoa Mwanza ndani ya operesheni Chanjo Kizazi kwa ushindi mkubwa

**Na Anthony Gervas,** Mwanza

MKOA wa Mwanza unaelezwa umefanikiwa kufikia asilimia 98.9 ya lengo la Chanjo ya Saratani ya Shingo ya Uzazi, kwa mabinti wenye umri kuanzia miaka tisa hadi 14 kwa mujibu wa Sera ya chanjo kitaifa.

Tangu kuanza chanjo hiyo mkoani humo, mwezi Mei mwaka huu, tayari Idara ya Afya imeshafanikiwa kuchanja mabinti 324,517, huku lengo lililowekwa ni kuwachanja mabinti 328,368.

Katika utekelezaji, kunatajwa kuwapo vituo 400 vimetengwa vya kutoa huduma hiyo kwa walengwa katika halmashauri zote nchni sasa.

Ni mafanikio yanayotokana na kuzinduliwa kitaifa chanjo ya saratani ya shingo ya uzazi mkoani Mwanza na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, miezi miwili iliyopita mwaka huu.

Inaelezwa kuwa, maambukizi ya virusi vya saratani ya mlango wa uzazi kwa mabinti au wanawake, hutokana hasa kufanya tendo la ndoa na mwanaume ambaye hajafanya tohara, hata akatunza virusi hivyo katika sehemu za haja ndogo.

### MRATIBU CHANJO

Mratibu wa chanjo Mkoa wa Mwanza, Amosi Kiteleja anasema chanjo hiyo ni endelevu kupitia Sera ya Taifa, serikali ikilenga kufikia hadi Disemba mwaka huu 2024, mabinti wote wa umri huo wawe wameshafanyiwa chanjo hiyo.

Kiteleja anasema, lengo hilo linakusudiwa ifikapo mwakani, mabinti watakaoendelea kuchanjwa ni wenye umri wa miaka tisa pekee, kutokana na matokeo ya utafiti wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)mkoani Mwanza.

Kiteleja anasema, dozi ya chanjo itapunguzwa kutoka mbili hadi tatu na kubaki moja tu, ambayo kiwango chake cha kuzuia maambukizi ya saratani ya shingo ya uzazi kitakuwa sawa na dozi tatu za awali.

Lengo la serikali kuwapatia chanjo mapema mabinti wakiwa na umri wa miaka tisa, ni kuwakinga kupata maambukizi ya virusi hivyo, kabla hawajaanza vitendo vya kujamiiana.

Utoaji wa huduma hizo unafanyika kwa ushirikiano na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kutoka mkoani Mwanza, kupitia kitengo cha utafiti MITU.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akishuhudia uchanjaji saratani ya shingo ya kizazi, Aprili mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

> **Dozi ya chanjo itapunguzwa kutoka mbili hadi tatu na kubaki moja tu, ambayo kiwango chake cha kuzuia maambukizi ya saratani ya shingo ya uzazi kitakuwa sawa na dozi tatu za awali.**



Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Mwanza, Amosi Kiteleja akiwa ofisini kwake jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

Halmashauri zimetengewa vituo vya kutoa huduma ya chanjo bila malipo katika mkoa huo, ili kuhakikisha kila mlengwa anafikiwa. Hapo inahusisha halmashauri za: Ilemela, Nyamagana, Magu, Kwimba, Misungwi, Sengerema, Buchosa na Ukerewe.

Kiteleja anatahadharisha kuwa, endapo mabinti au wanawake hawatapata chanjo mapema ya kinga ya kuzuia maambukizi hayo, athari zake zinaweza kusababisha hata vifo, familia kutumia gharama kubwa kupata matibabu na kutumia rasilimali nyingi, kuyumba kiuchumi, pia kukabiliwa na umaskini.

### MGANGA MKUU WA MKOA

Dk. Thomas Ruchunzibwa, ni Mganga Mkuu Mkoa wa Mwanza, anayeshukuru serikali kwa ushirikiano wake na taasisi za utafiti mbalimbali, ikiwamo

NIMR ambao umeonyesha matokeo ya ufanisi katika chanjo hiyo.

Dk, Ruchunzibwa anasema kuwa dalili zinaonyesha mama aliyepata kinga mapema akiwa binti kabla hajaingia kwenye ndoa au kuanza kujamiiana anakuwa na uwezekano mkubwa wa kutokuwa na Saratani ya shingo ya uzazi,dhumuni lake ni kulinda kundi zima la jinsia ya kike.

Takwimu zinaonyesha kuwa mama akishapata maambukizi ya virusi hivyo,uwezekano wa kumkinga baadaye au kumtibu unakuwa haupo.

'Kwa mujibu wa utafiti wa Taasisi yaTaifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu(NIMR)uwezo wa dozi moja ni ule ule sawa na dozi tatu au mbili,hivyo mwakani mabinti watakaoendelea kuchanjwa ni wale wenye umri wa maka 9 tu,anasema Dk,Ruchinzibwa.

Anasema kuwa jambo muhimu ni kuwashawishi na kuwashauri mabinti kuendelea kupata chanjo hiyo ambayo haina madhara yeyote kwa afya ya binadamu, hakuna gharama za kuchangia mwananchi bali haina malipo.

Anawaomba viongozi wote wa dini,siasa kuelimisha jamii, waumini na wanachama wao kwenda kupata chanjo katika vituo vya afya vilivyotengwa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo mkoani Mwanza.

### MZIZI WA CHANJO

John Changalucha ni mtafiti mwandamizi katika Taasisi ya taifa ya utafiti wa magonjwa ya Binadamu (NIMR) kupitia kitengo cha MITU, ambao wamekuwa wakishiriki utafiti wa chanjo ya kuzuia Saratani ya Shingo ya Uzazi tangu mwaka 2007.

Anasema sababu ya kuanza utafiti huo wa chanjo hizo, ni kwamba mwaka 2006 ziliidhinishwa na kuanza kutolewa leseni kwa ajili ya kutumika sehemu mbalimbali duniani, lakini bahati mbaya utafiti huo haukuanza kutumika awali katika nchi za Afrika.

Hivyo, kukawapo maswali kuhoji uwezo ulioonekana kwenye hizo chanjo katika nchi za Ulaya na Marekani, iwapo ungekidhi mahitaji ya Afrika, kwa sababu yapo maambukizi mengine yanayoweza kuathiri utengenezaji wa kinga kwa mhusika.

Katika kujibu swali hilo utafiti wao kwanza ulilenga kutathmini kama hizo chanjo zinaweza kuwa salama,lakini vile vile zinaweza kutengeneza kinga inayoweza kuzuia Saratani ya Shingo ya kizazi,hivyo utafiti huo walifanya hadi 2010,wakishirikisha wanawake kuanzia umri wa miaka 10 hadi 25.

Katika utafiti wao, waliona chanjo hizo ziko salama na kinga iliyotengenezwa zilikuwa kubwa kwa wasichana wadogo kuanzia umri wa miaka 10 hadi 14, ikilinganishwa na wanawake wa umri wa miaka 15 hadi 25. Ni matokeo yameonekana katika utafiti uliofanyika Ulaya na Marekani.

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Kambi Makonda ilivyomuunga mkono Samia

INATOKA UK.11

ja alinipigia simu, akaniambia unaweza kwenda na huyo mtoto tukikusaidia? Nikamuambia 'naweza kwenda'. Akaniambia nijiandae. Nikaenda kwa mama kuomba unga na mchele, ili tuweze kupata chakula tunavyosafiri," anasimulia

Joyce anaeleza taarifa zake zinajulikana kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kuhusiana na tatizo lake na wasaidizi wake walimjulisha aandike barua ili serikali imsaidie tiba, lakini mpaka sasa hajatibiwa.

Anasimulia kwamba vipimo alivyofanyiwa mtoto wake, kipo kilichobaini uti wa mgongo umeathirika, jambo ambalo hakujua.

"Nyumba zote nilizopanga nafukuzwa, kwa sababu mtoto ananuka na nzi wanamfuata. Sasa nimeona nuru, mwanangu hajawahi kupimwa kwenye hiki kipimo kikubwa ni kwa mara ya kwanza, Mungu ameniona," anasimulia, huku akitokwa na machozi.

### WAKAZI ARUSHA

Dorah Mollel, ni mkazi wa Arusha anasimulia alikuwa na shida ya macho na nyonga tangu mwaka jana, akiwa ameanza matibabu hakupata nafuu.

"Nimejikuta sina uwezo wa kuendelea kujitibu tangu Disemba mwaka jana. Ninaugua na huu mguu ulikufa ganzi, natembea kwa kuchechemea.

"Ninashukuru kwa msaada huu kwa kuwa sijawahi kupata msaada wa aina hii ninamshukuru Makonda kutuletea haya matibabu," anasema.

"Hatukuwa na uwezo wa kumkaribia mkuu wa mkoa na kueleza kero, lakini sasa hivi tumefunguliwa, tunaenda kuongea naye na hata kwa Mkuu wa Wilaya na kueleza shida zako na kusaidiwa," anaeleza.

"Hawa watu wote tumekuja kufurika hapa uwanjani ni kwamba hatuna fedha kwa ajili ya kujitibu. Unaambiwa unatakiwa kutibiwa kwa Sh milioni 1.5. Kama mimi nisingeweza kipimo cha mwisho, niliambiwa nitoe Sh 100,000 nilikosa nikarudi nyumbani.

"Nilivyosikia hii kambi nikaja mbio, huu umati wanaugua, hawana sehemu ya kwenda kuomba msaada na hospitali zetu zinahitaji fedha," anasema

Mollel anaeleza kwamba mhusika kafanyiwa kipimo cha macho na kupatiwa miwani, ameenda kupimwa nyonga ana amepatiwa matibabu.

"Tunakutana na madaktari wazuri ambao wanatusikiliza vizuri. Nimefanyiwa kipimo cha X-Ray bila ya malipo na dawa nimepatiwa. Ninamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozifanya za kutetea wananchi wanyonge," anasema.

Mwingine ni Mary Lyakurya, anayesimulia changamoto yake ya tumbo tangu mwaka 2021, akiambiwa anatakiwa kufanyiwa kipimo kwa gharama Sh. 600,000 na hakuwa nazo.

Anasema hakuwa vizuri kifedha, hata ikamlazimu kubaki nyumbani akiugua maumivu, mpaka alipopata taarifa ya kuwapo kambi yenye matibabu bure. Anaikumbuka siku ya tarehe 25 mwezi uliopita, majira ya saa 11.00 alfajiri akahudhuiria na kupewa namba 39, ila alishindwa kupata matibabu siku hiyo kutokana na foleni, licha ya kuwahi.

"Sikukata tamaa, Jumanne nikafika nikaonana na madaktari husika walinifanyia matibabu na kunipatia rufani niende hospitali ya Mount Meru, wakanifanyia uchunguzi na kunipangia Juni 28 nirudi wanifanyie kipimo," anasema.

Anasema, vipimo vya awali vilionyesha kuwapo uvimbe kwenye utumbo, akajulishwa anachukuliwa nyama za kupelekwa maabara kuchunguzwa zaidi.

"Nimeambiwa Julai 1 nikachukue majibu. Kwa kweli ninamshukuru Mungu na Rais Samia, kwa sababu wengi ni wagonjwa tunakosa huduma kutokana na gharama za matibabu kuwa kubwa," anasema

Mkazi wa Arusha, Raymond Gabriel, anasema, alikuwa kazini wakivunja ukuta, ukamuangukia akawa amekatika mguu wa kulia na mgongo kuvunjika pingili tatu.

Anasema, alikaa Hospitali ya Rufani Mount Meru kwa siku tano akisubiri fedha za kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC, huku mguu ukiharibika.

Gabriel anasema, bosi wake alitoa Sh. 500,000 za gari la wagonjwa kumsafirisha na alivyofika hospitalini KCMC mguu wake ulikuwa tayari umeoza, wakaanza kumfanyia oparesheni.

Anasema tiba y uti wa mgongo kufanyiwa upasuaji ilishindikana kwa kukosa fedha Sh. Milioni 10, hata mguu wake alitibiwa baada ya kuuza kiwanja chake, kwani bosi wake baada ya kumpatia usafiri, hakurejea tena kunihudumia,"anasema.

Gabriel anaeleza kuwa baada ya kufika katika kambi hiyo, daktari alimfanyia vipimo, pia akakutwa na shida nyingine ya kupata choo kikubwa na kidogo, kutokana na tatizo la uti wa mgongo lililompata.

Anasimulia alikofikia ni kwamba, ameshafanyiwa kipimo cha gharama ya Sh. milioni 1.5, iliyokuwa inamsumbua tangu mwaka juzi akikosa fedha nza tiba na dawa.

Ni aina ya mfumo unaoacha salamu za nafasi ya Bima ya Afya kwa Wote.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha. Paul Makonda, akijumuika na umma, katika kampeni ya tiba bure za kibingwa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha. **PICHA: BEATRECE SHAYO**

## Mkoa Mwanza ndani ya operesheni Chanjo Kizazi kwa ushindi mkubwa

INATOKA UK.12

Changalucha anasema, walitoa matokeo hayo kwenye Wizara ya Afya, kuwa chanjo hizo ni salama zinaweza zikatumika, kilichobaki ni namna ya kutolewa, kwa sababu umri ulioelengwa haukuwa sahihi, chanjo zikazotolewa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, badala ya wasichana wa umri miaka 9 hadi 14.

Hivyo, ikatakiwa nchi zitengeneze mfumo ambao zinaweza kuwafikia wanafunzi walioko shuleni na hilo lilileta changamoto,sababu ilihitaji kuwa na fedha za kutosha,vilevile wafanyakazi wa afya kwenda kutoa huduma mashuleni.

Wakati wa utoaji chanjo hizo wapo walioishia dozi moja na mbili na wengine kufikisha tatu,k ilichofanyika ni kufuatilia wote ili kuona kiwango cha maambukizi katika waliopata dozi moja, mbili na tatu.

Anataja, ikawa bahati nzuri matokeo ya ufuatiliaji yalionyesha kwamba wasichana au wanawake waliopata dozi moja walikuwa wamekingwa dhidi ya maambukizi sawa na waliopata dozi mbili au waliopata tatu.

Matokeo hayo yaliwapa nguvu ya kuweza kufanya utafiti wao walioufanya mkoani Mwanza, ili waweze kujibu swali walilokuwa wakiulizwa je dozi moja ya chanjo inaweza ikatengeneza kinga ambayo inayoweza kuzuia saratani ya shingo ya uzazi.?

Ili kuweza kujibu swali hilo, anasema wakashirikisha wasichana wapatao 930 wa shule za msingi, sekondari kidato cha kwanza na cha pili katika shule za kutwa kwa maana kwamba iwe rahisi kuwapata wazazi wao waweze kutoa ridhaa ya kutoa chanjo kwa watoto wao.

Anasema kinga moja ya saratani ya shingo ya uzazi, inazuia virusi kwa kiwango cha asilimia 97, ikiwa ni kiwango cha saratani kwa wanaume sio kikubwa kama cha wanawake.

### KUTOKA WHO

Shirika la Afya Duniani (WHO)linasema ifikapo mwaka 2030 tatizo la saratani ya shingo ya uzazi liwe limekwisha,wasichana wengi watakuwa wamepata chanjo.

Tayari imeshaanza kutoa chanjo kwa wavulana katika wilaya nne Magu,Kwimba,Sengerema na Misungwi kwenye kata 26 zilizogawanywa 13 wavulana na 13 zingine wasichana.

Baada ya miaka miwili au mitatu, wanatarajia kupima katika kata zote, ili kulinganisha kiwango cha maambukizi pande zote mbili wasichana na wavulana pia kutoa majibu ya swali kwa wananchi pia serikali.

Kama kiwango cha maambukizi upande mmoja kitakuwa kikubwa wataiambia serikali na kutoa majibu ya swali la wananchi au jamii lililoulizwa kwamba kwanini wavulana hawapatiwi chanjo za kuzuia maambukizi ya virusi hivyo.

AFYA

# Wizara Mifugo, Uvuvi inavyozamia utafiti chanjo kunusuru binadamu kuambukizwa

**Na Christina Haule**, MOROGORO



Mifugo; mbuzi na kuku ikiwa inahudumiwa. Kampeni ya kiserikali inayoendelea ni kuwachanja, ili kupata usalama wao na binadamu kiafya. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

KATIKA mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka wa fedha ulioko, serikali imetenga shilingi bilioni 29 za kuanzia kampeni ya chanjo ya mifugo kitaifa, ili kudhibiti magonjwa ya wanyama kwenda kwa binadamu nchini.

Ni ufafanuzi wa Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini, Tanzania Dk. Benezete Malinda, katika mahafali ya kundi la wataalam 30 katika mafunzo ya miezi minne ya mifugo kwa vijana yaliyofanyika kwenye Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), yaliyoandaliwa na Shirika la Kilimo na Chakula (FAO).

Dk. Malinda anasema, chanjo hizo zinatolewa katika mwaka wa fedha 2024/25, kuanzia mwezi huu, ukigusa mifugo ya ng'ombe na mbuzi, sambamba na kuhakikisha chanjo za kichaa cha mbwa zilizokuwa kwenye hatua mbalimbali za utengenezaji zinakamilika.

Anasema chanjo hizo zitawafikia zaidi ya ng'ombe milioni 17, mbuzi na kondoo milioni 17 na zaidi ya kuku milioni 40, hatua inayotarajiwa kufanyika kwa gharama za serikali, wafugaji hawatagharimia chochote.

Rai yake Dk. Malinda, anawaomba wafugaji na wananchi kwa, kuandaa sehemu za kuchanja, ili litakapofika wakati mwafaka, sehemu hizo ziwe tayari kwa utambuzi na uchanjaji mifugo na wanyama watakaochanjwa, wanavalishwa heleni kutambulika na wakati huohuo, kusaidia kukidhi masoko ya kimataifa.

Anasema hali ya chanjo kwa sasa nchini imeimarika, baada ya serikali kuweka mazingira mazuri ya uzalishaji wa chanjo nchini na mpaka sasa, kuna viwanda vitatu vinavyozalisha chanjo za mifugo.

Anavitaja viwanda hivyo, kuwa ni pamoja na chombo cha kiserikali kitwacho Vaccine Institute kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani, ambacho kimefikia kiwango cha kuzalisha chanjo aina saba.

Dk. Malinda anakitaja kiwanda kingine binafsi kinachojulikana kama Esta Bio- Sayansi, kilichopo Kibaha mkoani Pwani, kimefikia kiwango kinazalisha aina nane tofauti; pia Novabi cha mkoani Morogoro, kinachozalisha chanjo kuu aina ya tatu, zenye zinazokidhi mahitaji ya nchini.

"Sisi kama nchi, magonjwa 'tuliya -group' (kuyatenga) kwenye eneo moja la magonjwa ya kipaumbele, ambayo yanaaathiri biashara za kimataifa na za kikanda lakini yanayotoka kwa Wanyama kwenda kwa binadamu.

"Kama serikali, tulikuja na magonjwa 13 na kati ya magonjwa hayo, tuna uzalishaji wa chanjo aina saba hadi nane. Serikali imetoa msamaha wa kodi kwa dawa na chanjo za mifugo ambazo hazizalishwi ndani ya nchi na tunapozihitaji, serikali inatoa kibali na chanjo zinaingizwa nchini" anaeleza Dk. Malinda.



### UGONJWA SOTOKA

Kuhusu ugonjwa sotoka, Dk. Malinda anaeleza unawapata zaidi mbuzi na kondoo amna serikali huchukua hatua, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, ikiwamo Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) la Umoja wa Mataifa, sasa wapo ikiwa katikia katika hatua ya kuutokomeza ugonjwa.

"Kwa hali tuliyoifikia, serikali inapaswa kuandaa nyaraka kwa ajili ya kuwasilisha Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, ili kuomba kibali cha kutangazwa Tanzania ni huru kutokea kwenye ugonjwa wa sotoka," anasema.

Anasema, ugonjwa huo una magonjwa yasiyo na mipaka na kuweza kuathiri soko la ndani na nje, kwa sababu una uwezo wa kuua mbuzi na kondoo kwa asilimia 100 na umekuwa kwa zaidi ya miaka 10 hadi 15, Tanzania baada ya kuingia katika nchini kati a moja zinazoizunguka.

"Matokeo ya maabara ya miaka mitano iliyopita, inaonyesha ugonjwa huu umetokomea nchini kwa kiwango kikubwa na tulipofanyiwa utafiti za Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, imeonekana tumeshavuka hatua ya kwanza na ya pili," anafafanua Dk. Malinda.

Anaendelea: "Tupo hatua ya mwisho ya tatu, ya kuutokomeza ugonjwa huo na tunasubiri kibali cha kutangaza umekwisha.'

### MUSTAKABALI UTAFITI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe, anawaelekeza wahitimu hao kuhakikisha wanaweka kwa ufupi tafiti zao 30 katika kitabu kimoja, ili kusaidia kufahamu watafiti na tafiti kwa maendeleo ya nchi.

Profesa Shemdoe anasema, ni hatua inayobeba maana ya kuondoa magonjwa ya wanyama kwenda kwa binadamu na kuiletea faida nchi katika biashara kimataifa.

> **"Utafiti aliyoufanya kuanzia mwaka jana, huko Unguja, amebaini ni ugonjwa unaosababishwa na mbwa wazururaji na inapaswa kutafutwa namna sahihi ya kuwachanja.**

Anasema upatikanaji wa taarifa za mifugo kutoka wilayani, unasaidia upangaji bajeti kuanzia kwenye halmashauri, mikoa hadi taifa, hata bajeti sahihi kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mwakilishi kutoka FAO, Dk. Nyabenyi Tipo anasema programu ya kuwajengea uwezo vijana, inawaletea maendeleo katika rasilimali mifugo na kusaidia kupunguza umaskini na majanga duniani.

Anasema uwekezaji katika afya na ulinzi kwa wanyama kitaifa na kimataifa, unasaidia kuboresha hali za wanyama na kuleta tija hasa kwa masoko ndani na nje ya nchi. Mwanachuo aliyetafiti kichaa cha mbwa, Fatma Abdulah, anasema tahadhari za kuzuia ugonjwa huo zinahitajika mapema, ili kukomesha ugonjwa na hatari hiyo kwa afya ya mbwa na binadamu kwa ujumla.

Anasema utafiti aliyoufanya kuanzia mwaka jana, huko Unguja, amebaini ni ugonjwa unaosababishwa na mbwa wazururaji na inapaswa kutafutwa namna sahihi ya kuwachanja.

Mkurugenzi Rasilimaliwatu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Mhina, anawasisitiza vijana waliopata mafunzo hayo wazingatie na kuwachanja kwa usahihi mifugo, kulingana na chanjo husika, ili kudhibitia madhara tajkwa.

"Sasa najua hamtaenda kuchoma sindano zile za chanjo kwenye nyama au kwenye mifupa, zile ambazo zinapaswa kuchanjwa kwenye Ngozi, mtaenda kufanya hivyo na mifugo yetu haitaenda kuota majipu," anasema.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA MPANGO WA KUWAWEZESHA VIJANA KIUCHUMI KUMBUKUMBU NA: 00000548

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD) inaalika makampuni au taasisi yenye uzoefu na sifa nzuri kuonyesha nia kwa ajili ya mpango wa kuwawezesha vijana kiuchumi kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Kampuni ya EACOP inajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
EACOP inatarajia kutoa mpango wa uwekezaji wa kijamii kwa hiari katika jamii zilizoathirika na EACOP. Mpango mmoja unaozingatiwa ni kuwawezesha vijana kiuchumi. Muundo unaweza kujumuisha, lakini sio tu:

- Kutambua idadi na jamii lengwa/ zitakazonufaidika
- Kutambua wanufaika
- Kutambua fursa za kuunganishwa na masoko
- Kuandaa programu ya mafunzo na kujenga uwezo kuhusu stadi za maisha, ujuzi wa kiufundi, ujuzi wa ufundi, na stadi za kupata ajira - kwa kutumia miundo iliyopo na mafunzo ya kibunifu .
- Muundo wa programu unapaswa kuzingatia mahitaji na maslahi maalum ya wanawake vijana
- Kurahisisha ufikiaji wa programu za kuimarisha ujuzi endelevu zinazotolewa na taasisi nyingine za kibinafsi na za umma
- Kurahisisha ufikiaji wa mikopo
- Kufanya ufuatiliaji, mafunzo na msaada endelevu

**VIGEZO MUHIMU:**
**Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:**

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, ujuzi kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA).
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana ikiwa ipo.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ametuma maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP Database) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani (Compliance with Petroleum Local Content Regulation,2017)
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

---

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 21/07/2024. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **EOI 00000548: Kuonesha nia kwa ajili ya mpango wa kuwawezesha vijana kiuchumi.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

---

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makumpuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## IMERUDIWA: MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA KWA JAMII MAALUM ZA MAKUNDI YA PEMBEZONI WANAOJITAMBULISHA KAMA WATU WA ASILI KUMBUKUMBU NA: REQ-00000513

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD) inaalika makampuni au taasisi yenye uzoefu na sifa nzuri kuonyesha nia ya kutoa huduma kwa jamii maalum za makundi ya pembezoni wanaojitambulisha kama Watu wa Asili kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Kampuni ya EACOP inajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
Kampuni ya EACOP inapita na imetwaa ardhi katika takribani jamii 30 za makabila ya pembezoni yanayojitambulisha kama watu wa Asili katika mikoa ya Tanga, Manyara, Dodoma na Tabora. Kama sehemu ya ahadi yake kwa jamii hizi zilizorejelewa katika mikataba mbalimbali na kwa kuzingatia Viwango vya Fedha vya Kimataifa, EACOP sasa inatafuta taasisi zenye uzoefu na sifa nzuri kutoa huduma kwa jamii hizi maalum za makundi haya ya pembezoni wanaojitambulisha kama Watu wa Asili (maelezo yatatolewa wakati wa wito wa zabuni):

- 00000513 -01: **Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi:** shughuli zitajumuisha kuwajengea uwezo katika mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji; kurahisisha mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji; kusaidia kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi; kurahisisha upatikanaji wa CCROs;
- 00000513 – 02: **Kuimarisha Uwezeshaji wa Wanawake na Vijana** kupitia kuunda vikundi na kukuza mazingira bora ya biashara kwa vijana na wanawake pamoja na kutambua fursa za kuunganisha vikundi vya vijana na wanawake na taasisi zinazotoa msaada wa ujasiriamali husika.
- 00000513 – 03: **Kuimarisha Jamii:** Kuunda na kuimarisha Kamati za Maendeleo ya Jamii ya Kijiji na kutekeleza shughuli za kuwajengea uwezo katika ngazi ya jamii.

Katika kufanya kazi hii, EACOP inahitaji taasisi moja au zaidi (za kibinafsi au zisizo za kiserikali) zenye rekodi thabiti ya uzoefu katika kufanya kazi na jamii hizi kuhusu masuala haya.
**Muombaji anaweza kuomba vipengele vyote tajwa au akaomba kipengele kimoja au viwili kulingana na uwezo wake.**

**VIGEZO MUHIMU:**
Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, ujuzi kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA).
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana ikiwa ipo.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ametuma maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP Database) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani (Compliance with Petroleum Local Content Regulation,2017).
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.

---

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 17/07/2024. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **REQ-00000513: Maombi Ya taarifa ya Kuonesha nia Kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii maalum za makundi ya pembezoni wanaojitambulisha kama watu wa asili.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

---

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.



# DC atoa siku 4 kampuni ya chai kulipa wafanyakazi

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, ameuagiza uongozi wa kiwanda cha chai (kampuni ya chai ya DL Group) kulipa malimbikizo ya mishahara kwa wafanyakazi wake ndani ya siku nne.

Alitoa agizo hilo kufuatia mgomo wa wafanyakazi wa viwanda vya Kibena, Luponde na Ikanga-Lupembe ambavyo vyote vipo wilayani Njombe.

Aidha sababu ya mgomo huo ni kuchelewa kwa mishahara yao kwa kipindi cha miezi mitano pamoja na mwajira kutopeleka michango katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii NSSF tangu mwaka 2019 ambayo ni Sh. bilioni 1.3.

Kissa alisema serikali haifurahishwi na mambo yanayofanywa na kampuni hiyo kwa sababu kumekuwepo na migogoro hiyo mara kwa mara bila ya kufika mwisho.

"Mimi mwenyewe nimekuja hapa Njombe mwaka 2021 katika changamoto kubwa katika Wilaya ya Njombe ni suala la chai. viwanda hivi vitatu vya huyu DL kwa hiyo tatizo siyo chai tatizo ni DL Group, serikali haiwezi kubali lazima ifanye maamuzi magumu maana hapa sasa imefika mwisho," alisema Kasongwa.

Awali Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi TPAWU Luponde, Hashim Ramadhan alisema wafanyakazi hao wanadai mishahara ya miezi mitano.

Alisema mwekezaji huyo ametelekeza mashamba hali ambayo inaweza kusababisha kushusha thamani ya zao la chai.

Anastazia Mwapinga aliomba serikali kuingilia katika suala hilo akisema limekuwa likijirudia mara kwa mara na kueleza kuwa hata maisha yao ni magumu kwa sababu wametoka mikoani ili kuja kufanya kazi kwa ajili ya kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Nao wawakilishi wa uongozi wa kampuni ya DL Group akiwemo Mhasibu wa Kampuni, Patrick Mwigune alisema sababu kubwa ya kuchelewa kulipa madeni hayo ni kutokana na zao la chai kushuka thamani.

Alisema: "Hata mimi nadai miezi 10, zao la chai limeshuka thamani na hata hela kidogo ambayo tunapata kutokana na mauzo kuna madeni mengi kama umeme tumekuwa tukilipa huko".



Mkazi wa Jiji la Mbeya, akivuta mkokoteni uliosheheni mzigo wa magurudumu, ili kujipatia ujira wa siku, katika eneo la Uwanja wa Sokoine juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Vijana kujadili fursa za masoko, uzalishaji kilimo

**Na Gwamaka Alipipi**

VIJANA zaidi ya 100 wanatarajia kukutana na kujadiliana namna ya kujenga mazingira wezeshi ya ujasiriamali, fursa za masoko, pamoja na na uzalishaji katika kilimo.

Mkurugenzi Mkazi wa Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), Vianey Rweyendela, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kuelekea Mkutano wa Sera wa Vijana na Ubadilishaji wa Mifumo ya Chakula, utakaofanyika Julai 5, jijini Dar es Salaam.

Alisema mkutano huo utawakutanisha vijana, washirika wa utekelezaji, wadau muhimu katika mlolongo wa thamani ya mifumo ya chakula ili kujua mahitaji na vipaumbele ya vijana katika kilimo.

Alisema mkutano huo utafanikisha hatua za sera muhimu za kuwawezesha vijana katika kilimo, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuhakikisha mabadiliko katika mifumo ya chakula.

"Lengo la mkutano huo ni kuunga mkono ushiriki wa vijana katika mifumo ya chakula inayostahimili mabadiliko ya hali ya hewa na hati ya kumbukumbu ya michango ya vijana katika kuimarisha na kukuza programu zinazolenga vijana." alisema Rweyendela.

Alisema mada zitakazojadiliwa ni pamoja na upatikanaji wa ardhi, fedha, huduma za maendeleo ya biashara, utetezi wa sera, na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Hivyo, aliwahimiza vijana kushiriki, kuchukua fomu katika jukwaa la kidijitali la AGRA.

Mratibu wa Programu ya BBT, kutoka Wizara ya Kilimo, Vumilia Zikankuba, alisema wizara ina lengo la kutoa mwongozo wa sera na huduma kwa mfumo wa kilimo na ushirika ulioimarishwa kibiashara, wenye ushindani na wenye ufanisi.

Alisema: "Serikali inajitahidi kutoa huduma za kilimo na ushirika zenye ubora, kutoa mazingira mazuri kwa wadau, kuimarisha uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa na kuwezesha sekta binafsi kuchangia kwa ufanisi katika uzalishaji endelevu wa kilimo, tija na maendeleo ya ushirika".

# Waanzisha kiwanda kuuongezea thamani mpunga

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

WAKULIMA wa mpunga kutoka Kijiji cha Azimio Mswiswi wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wameanzisha kiwanda cha kuchakata mpunga kwa lengo la kuongezea thamani kabla ya kuuza.

Mbali na kuanzisha kiwanda hicho pia wameunda kampuni iitwayo Azimio Mswiswi High Quality Rice Millers ili kurahisisha uendeshaji wa shughuli za kilimo ikiwemo ununuzi wa pembejeo na ugani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ghala la kuhifadhi mpunga na mashine ya kukoboa, Meneja wa kampuni hiyo, Herbert Mgome alisema wametekeleza miradi hiyo chini ya ufadhiri wa USADF.

Alisema katika kutekeleza mradi huo USADF, liliwapatia Sh. milioni 200 ambazo zilitumika kwa ajili ya kutoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi pamoja na wakulima kuhusu mbinu za uendeshaji wa kampuni hiyo.

Alisema fedha hizo pia zilitumika kuwafundisha wakulima mbinu za kilimo bora pamoja na kutembelea wakulima na kampuni za kilimo zilizofanikiwa ili wajifunze zaidi.

"Baada ya mafunzo haya shughuli zetu, shughuli za ugani zimeboreshwa ambapo wakulima wanasaidiwa mbinu mbalimbali za kilimo bora, pia kwa sasa kiwango cha kukopesheka kimepanda kutoka Sh. milioni 50 mpaka Sh. milioni 400," alisema Mgome.

Alisema baada ya kuboreshwa kwa shughuli za ugani hata kiwango cha uzalishaji wa mpunga kimeongezeka kutoka tani 1.2 mpaka tani saba kwa hekta moja.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni hiyo, Omary Mwambela aliiomba serikali kuwasaidia kutatua kero mbalimbali zinazowakabili ikiwemo kuboresha miundombinu ya barabara ili kuwarahisishia usafirishaji wa mazao yao.

Pia, alisema wakulima wanakabiliwa na tatizo la kutozwa ushuru wa mazao yao zaidi ya mara mbili ikiwemo wanaposafirisha kutoka shambani kwenda kuuhifadhi nyumbani akidai kuwa imekuwa kero kubwa kwao.

Hata hivyo, aliomba serikali kuwasaidia kuboresha huduma za maji na umeme ili shughuli zao ziende vizuri na watimize malengo yao ya kuwainua wakulima.

Akizindua mashine ya kukoboa mpunga na ghala la kampuni hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliishukuru USADF kwa ufadhili walioutoa kwa wakulima hao akidai kuwa umesaidia kuboresha kilimo kwa wananchi.

Hivyo, aliagiza taasisi mbalimbali za serikali kuboresha huduma muhimu kwenye eneo hilo ili miradi hiyo iendeshwe vizuri na wafadhili waione tija waliyokuwa wanaikusudia.

Aliagiza Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya kujenga barabara inayopita jirani na eneo la kiwanda hicho ili kuwasaidia wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi, huku akilitaka Shirika la Umeme (TANESCO) kuweka transfoma mpya kwenye kiwanda hicho.

Wilaya ya Mbarali ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa mpunga katika Mkoa wa Mbeya ambapo ndilo zao ambalo linazalishwa zaidi katika wilaya hiyo.



## Serikali kuunga mkono juhudi za wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema itaendelea kuunga mkono jitihada za wawekezaji katika sekta ya mifugo za kuleta maendeleo ya sekta hiyo nchini.

Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo alipofanya ziara ya kuangalia hatua za mwekezaji anayezalisha vifaranga vya kuku katika shamba hilo.

Alisema kuwa lengo la kuruhusu uwekezaji huo ni kuzalisha vifaranga vya kuku na kuwagawa kwa wafugaji wadogo kwa mkataba maalum ili waongeza tija katika shughuli zao.

Waziri Shamata alisema hatua hiyo imekuja baada ya serikali kuona haja ya kurudisha shughuli zake za ufugaji katika eneo la iliyokuwa Zanzibar Poultry Company (ZAPOCO) lilipo Dole, Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema kuwa eneo hilo litakua na uwezo wa kuwakomboa wafugaji wa kuku kwa kuongeza ufanisi kwenye uzalishaji wa kuku na bidhaa nyingine jambo litakaloongeza ajira pamoja na kuwalinda wafugaji wa Zanzibar.

Aidha, Shamata alisema kwa muda mrefu wafugaji hao wamekuwa wakihangaika kutafuta vifaranga vyenye ubora pamoja na chakula ambacho kina bei ambayo hawawezi kuimudu.

"Wizara yetu haiwezi kumzuia mtu asifanye shughuli za ufugaji kwani tulichoamua ni kuongeza ufanisi na kutanua wigo katika uwepo wa wawekezaji ambao wataenda katika mfumo wa kuwekeza uzalishaji mzuri wa kuku mama," alisema Shamata.

Hata hivyo, alisema kufanikiwa kwa jitihada hizo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM Ibara ya 146 (A) (i) pamoja na utekelezaji wa ahadi za serikali.

Mratibu wa mradi, Salum Mohd Ali, alisema lengo la kuanzisha programu hiyo ni kuisaidia serikali kukabili ukosefu wa ajira kwa vijana walio mitaani watakaopata ajira na siyo kusubiri ajira kutoka serikalini.

# Kusini Unguja kinara dawa za tiba asili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKOA wa Kusini Unguja umetajwa kuwa na utajiri mkubwa wa tiba asili kutokana na kuwa na mimea mingi ya dawa ya tiba asili ikilinganishwa na mikoa mengine ya Zanzibar.

Hayo yamesemwa Zanzibar na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti Zanzibar, Dk. Mayasa Salum Ali, katika kikao cha wadau wa habari kuhusu wajibu wa vyombo vya habari katika kuzingatia maudhui ya utangazaji kuelekea Uchaguzi Mkuu, kikao ambacho kimeandaliwa na Tume ya Utangazaji Zanzibar.

Alisema Zanzibar ina mimea 120 ambayo inatumika katika kutibu magonjwa mbalimbali na watu wengi hawafiki hospitali kwa matatizo madogo na wengi huishia katika jamii kutika kupata tiba asili.

Dk. Mayasa alisema ni vyema kuisimamia na kuiendeleza tiba asili katika hali ya usasa ili kuokoa maisha ya wananchi wanaosumbuliwa na matatizo mbalimbali ya kiafya.

Aidha, alisema dawa za mimea ni salama lakini sio kila mmea ni salama, kuna viwango na aina ya mmea, hivyo kitu muhimu ni kwamba dawa za mimea zitumike kwa kiwango kinachostahiki.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO), ilieleza kuwa kila nchi inapaswa kuimarisha tiba zake asili na mwaka 2008 Zanzibar ilifanikiwa kuunda Sheria ya Tiba Asili Namba 8 na lengo likiwa ni kusimamia tiba asili.

Alisema Zanzibar imesimamia mambo mbalimbali katika kusimamia tiba asili ambapo asilimia 90 ya wananchi wa Zanzibar wanaamini na kuitumia tiba asili na husaidia kujenga afya.

"Hatuwezi kuishi bila ya tiba asili na hii siyo kwa Zanzibar tu bali dunia nzima, kila jamii ina utamaduni wake tukienda kama nchi kubwa zilizoendelea duniani kama China, Urusi, India, Thailand wanatumia tiba asili," alisema.

Alisema Zanzibar kuna waganga wengi wa tiba asili ambao bado hawajajisajili na waliojisajiliwa hadi sasa ni 700.

Mrajis wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Zanzibar, Mohamed Mshenga, alisema ni marufuku kusafirisha dawa za tiba asili bila ya kuwa na kibali maalum kutoka baraza la tiba asili.

Alisema vyombo vya habari vinamchango mkubwa wa kuinusuru jamii kutokana na wimbi la upoteshaji na udanganyifu.

"Matangazo yote ya tiba asili yasiofuata utaratibu, miiko kisheria hayakubaliki, tunafahamu kwamba kupitia vipindi na matangazo kwenye vyombo vya habari kuna mgongano wa kimaslahi ndani yake, lakini tuzingatie manufaa ya jamii kwanza kabla ya manufaa yetu binafsi," alisema.

Naye Katibu wa Ofisi ya Mufti Zanzibar, Khalid Ali Mfaume, alisema baadhi ya watu wanafanya udanganyifu katika kutoa matibabu ya tiba asili jambo ambalo linaweza kusababisha madhara makubwa kwa jamii.

Alisema wanawake ni waathirika wakubwa wa kutapeliwa na watoa huduma hizo, hivyo aliwataka kutokuwa wapesi kushawishika na wahusika kuacha mara moja kwa sababu ni kosa kisheria.

Katibu wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdallah, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa wadau wa habari kutokana na kuwapo na upotoshaji mkubwa wa matibabu ya tiba asili kupitia vyombo vya habari.



Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Tanga na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Rajabu Abdallah (juu ya gari) akizungumza na wananchi pamoja na wanachama wa chama hicho, wakati alipowasili wilayani Muheza jana, akitokea mkoani Dodoma. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# CCM: Mazrui anaitendea vyema Wizara ya Afya

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimesema kimeridhishwa na utendaji kazi unaofanywa na Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, katika kutekeleza ilani ya uchaguzi katika sekta ya afya, ikiwamo kusimamia ujenzi wa nyumba za makazi ya wafanyakazi wa afya na madaktari visiwani Pemba.

Pongezi hizo zilitolewa na Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM katika sekta tofauti Zanzibar.

Mbeto alimpongeza Waziri Mazrui kwa kutekeleza ilani ya CCM ambayo inasisitiza umuhimu wa ujenzi wa nyumba za madaktari kwa ajili ya kupata makazi bora na hivyo kutoa huduma za matibabu kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, aliwataka viongozi wengine wa upinzani kuiga mfano wa Waziri Mazrui kujitokeza hadharani kusifu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 katika Wizara ya Afya kwani huo ndiyo uungwana.

"CCM kinaunga mkono kazi inayofanywa na Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, katika kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM katika sekta ya afya na kuwawezesha wafanyakazi na madaktari kuwa na makazi bora ya kudumu," alisema.

Alisema kwa muda mrefu wafanyakazi wa sekta ya afya ikiwamo madaktari walikuwa wakikabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa nyumba za kuishi wakati wanapohamishiwa kwenda Pemba.

Alisema tatizo hilo lilisababisha baadhi ya wafanyakazi na madaktari kuibuwa visingizio mbalimbali kukataa uhamisho wa kwenda Pemba kufanya kazi.

Mbeto alisema CCM Zanzibar kinaunga mkono kazi kubwa inayofanywa na Dk. Hussein Ali Mwinyi katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, kwamba baadhi ya wizara ikiwamo ya elimu na afya tayari malengo yaliyowekwa yamevukwa katika utekelezaji wa ilani.

Alisema katika sekta ya afya tayari hospitali 11 za ghorofa katika kila wilaya zimejengwa Unguja na Pemba zikiwa na huduma zote ikiwamo za wajawazito na watoto.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**LOWLAND LUCAS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3705-0102** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia IWIJI SECONDARY SCHOOL mwaka 2011 na cheti cha chuo cha ualimu daraja III A chenye namba ya usajili **E0597-0234** kilichotolewa na **MBEYA MORAVIAN TEACHERS COLLEGE** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/MBE/MBE/14491/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIAMU CHARLES CHAMARE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S **2953/0014** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIRETI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/32460/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN JOSEPH MSANGI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **HERO HUNTER 150 CC,** YENYE USAJILI NO. **MC 553 DGX,** CHASSIS NO.**MBLKCR025MGG01832,** ENGINE NO.**KC10EHMGG02876,** RANGI NYEUSI TAARIFA YA POLISI **PHQ/MWA/NYA/22794/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHAFII AMIRI MSUYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **VOLKSWAGEN** yenye namba **T 583 DGN,** CHASSIS NAMBA: **WVWZZZ9NZ7U028750** na ENGINE NAMBA: **BKYEA8750.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/46729/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH ENOCK MWAKYONDE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T751 AUF** CHASISI NAMBA **AT19/0033969** KWA YEYOTE ALIEIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/9511/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF NYAMAGANA DISTRICT AT MWANZA**

**CIVIL/CRIMINAL APPEAL NO 6373 OF 2024**

**BANK OF AFRICA (T) LTD PLAINTIFF/APPELLANT**

**VERSUS**

**JAGILI MGANGA KADASO**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for hearing/mention on the 15 day of July 2024 at 8:30 am before Hon A. SUMARI in the forenoon.

**YOU ARE** required to appear before this court without fail and you must produce all documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the court this 01 day of JULY 2024

SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE MWANZA

**TO BE SERVE UPON:**

1. **JAGILI MGANGA KADASO**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**PIENSIA FOCUS NGURUWE** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya **BOXER** zenye usajili namba **MC 656 DUT, MC576 DTU, MC 118 DSF na MC 625 DUT.** Kwa yeyote atakaezionа atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/133437/2024**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**PIENSIA FOCUS NGURUWE** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya **BOXER** zenye usajili namba **MC 325 DMR, MC 800 DMC, MC 122 DPL , MC 681 DMQ na MC 375 DQR.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/133631/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 198 LA 2024**

**ELIHURUMA THOMAS MREMA ....MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**TABITHA GIDEON MKUDE ......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**TABITHA GIDEON MKUDE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**ELIHURUMA THOMAS MREMA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 22/07 2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya ya Mh **J.W. SILLAS** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 13 Mwezi 06 .. 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai Na.34/2024**

**Jina la Mdai: SAMWEL NG'HUMBU**

**Jina la Mdaiwa:NG'WALU SHIJA LUSHEDA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA (Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa NG'WALU SHIJA LUSHEDA.**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake(Eleza hapa habariza Madai) Utekelezaji wa hukumu ya Shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya mahakama hii tarehe 05 Mwezi 7 Mwaka 2024 saa 2.00 asubuhi kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe juu yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 Mwezi 06 Mwaka 2024

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ROSE JAMES KILUVIA** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 530BSX na MC 702 BTX** kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/TAN/5803/2024**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**PIENSIA FOCUS NGURUWE** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya Boxer zenye usajili namba **MC 450 DSC , MC 280 DSF , MC 392 DTQ, MC 256 DSF.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/KIG/133235/2024**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**PIENSIA FOCUS NGURUWE** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya Boxer zenye usajili namba **MC 730 DRF , MC 164 DRG , MC 564 DMU, MC 316 DQC.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/KIN/133118/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA**
**MBINGA**
**SHAURI LA MAOMBI YA UTEKELEZAJI NO 14034 / 2024**
**(Lililotokana na Shauri la Madai Na. 12/2022 Mahakama ya Wilaya Mbinga)**
**KATI YA**
**AMSEK SECURITY SERVICE LIMITED ......MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**CHINA HENAN INTERNATIONAL CO OPERATION GROUP COMPANY LIMITED (CHICO LTD) ....... MJIBU MAOMBI**

**KWA: CHICO LTD**

Unaamuriwa kufika Mahakamani tarehe **09/07/2024** saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri la maombi ya utekelezaji tajwa hapo juu limepangwa kwa ajili ya kusikilizwa.

Imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **02/07/2024**

L.B MWAPEMELA
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA MBINGA

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

# Hungary yataka vita Ukraine kusitishwa

**KYIV,** Ukraine

WAZIRI Mkuu wa Hungary na Rais wa Umoja wa Ulaya, Viktor Orban ametaka kusitishwa kwa mapigano kati ya Russia na Ukraine katika kuharakisha mazungumzo ya Amani.

Akizungumza baada ya kukutana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza nchini humo, alisema ni wakati wa kumaliza vita hiyo iliyoanza 2022.

Orban amekuwa mkosoaji kwa nchi za Magharibi kwa uungaji mkono Ukraine na kiongozi pekee wa Ulaya aliye karibu zaidi na Rais wa Russia Vladimir Putin.

Ziara hiyo ni ya kwanza kufanya nchini Ukraine katika kipindi cha miaka 12, ingawa alikutana na Rais Putin mara kwa mara.

Wakati wa mkutano wake na Rais Zelensky, hakukuonekana kuwa na wasiwasi wowote kati yao, lakini hakujibu maswali kutoka kwa vyombo vya habari baada ya kutoa taarifa zao.

Awali, Orban alipunguza makubaliano ya mfuko wa msaada wa Euro bilioni 50 uliotengwa kusaidia Ukraine.

Miezi sita ijayo anaanza nafasi yake kama mkuu wa Baraza la Ulaya, hivyo atakuwa na jukumu kubwa kama kiongozi wa Ulaya.

Kiongozi huyo, alifanya ziara Ukraine katika kufanya majadiliano, alisema kuna haja ya kusuluhisha kutoelewana kati ya nchi hizo mbili kwa kuzingatia siku zijazo.

Katika taarifa yake baada ya mkutano huo Zelensky alisema ni muhimu kwa Ukraine kuungwa mkono na Ulaya kuendelea kutoa kiwango cha kutosha cha misaada.

"Ni muhimu kwa ushirikiano kati ya majirani wote barani Ulaya kuwa wa maana zaidi na wa kunufaishana".alisisitiza Zelwnsky. **BBC**

# Wagombea Iran wachuana vikali

**TEHRAN,** Iran

WAGOMBEA wawili wa urais wa Iran juzi walikabiliana katika mdahalo wa pili na wa mwisho kabla ya duru ya pili ya uchaguzi utakofanyika Ijumaa ya wiki hii.

Wagombea hao Masoud Pezeshkian na Saeed Jalili, walijadili athari za vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa na Marekani na mataifa mengine ya Magharibi na kuwasilisha mipango yao kuhusu kufufua mkataba wa nyuklia na mataifa yenye nguvu duniani.

Mdahalo huo uliwakutanisha mwanamageuzi asiyejulikana sana Pezeshkian na Jalili ambaye ni mpatanishi wa zamani wa masuala ya nyuklia mwenye msimamo mkali watachuana katika marudio ya uchaguzi ili kumpata mshindi.

Iran itafanya duru ya pili ya uchaguzi wa ikiwa ni mara ya pili tangu Mapinduzi ya Kiislamu ya mwaka 1979.

Wapiga kura silimia 39.9 pekee walijitokeza kushiriki duru ya kwanza ya uchaguzi wiki iliyopita. **DW**

# Viongozi Marekani wajiuzulu

**WASHINGTON,** Marekani

WAKATI mbio za kuwania nafasi ya urais nchini Marekani zimeanza, Rais Joe Biden, ameanza kukumbana na vikwazo baada ya maofisa wakuu 12 kujiuzulu kupinga sera ya nchi hiyo katika vita ya Gaza.

Viongozi hao wametia saini waraka wa pamoja ambao unaeleza kwamba hatua za serikali katika kukabilana na vita hiyo, zimehatarisha usalama wa taifa la Marekani.

Ulisema kwamba sera za utawala wa Biden zimevuruga zaidi eneo hilo nakurejesha nyuma malengo ya Marekani.

Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani hapo awali ilikanusha madai hayo, ikihofia ukosoaji wa kujeruhi raia Ukanda wa Gaza na juhudi zake za kuimarisha misaada ya kibinadamu.

Taarifa ya pamoja ya maafisa hao wa zamani ilisema kuwa njia ya kidiplomasia ya Marekani na kuendelea kuipa silaha Israel kumehakikisha ushiriki wa taifa hilo usiopingika katika mauaji na usababishaji wa baa la njaa kwa wakazi wa Palestina waliozingirwa na wanajeshi wa Israel.

Kauli hiyo si ya kwanza kuzungumzwa na maofisa wa zamani, lakini safari hii inakuja sambamba na kujiuzulu nyadhifa zao.

Maryam Hassanein, msaidizi maalum katika Idara ya Mambo ya Ndani ya Marekani, pia alitia saini taarifa hiyo alisema sera hiyo iliyofeli ina madhara makubwa.

Maafisa hao wa zamani waliishutumu serikali ya Marekani kwa kung'ang'ania sera hiyo ambayo ni mbaya kwa watu wa Palestina lakini imehatarisha maisha ya Waisrael, kukandamiza uhuru wa kujieleza na kudhoofisha uaminifu wa Marekani juu ya kujitolea kwake kwa utaratibu wa kimataifa unaozingatia sheria.

**BBC**



Wanajeshi wa Israel wakifanya uvamizi katika kambi ya wakimbizi ya Nour Shams iliyoko Tulkarm, katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa na Israel jana. **PICHA: Reuters**

# Putin, Jiping kujadili ushirikiano

**ASTANA,** kazakhstan

VIONGOZI wa Russia na China wamewasiri nchini Kazakhstan, kuhudhuria mkutano wa kikanda wenye lengo la kuiongezea nguvu ushawishi wa kimkakati ya Asia ya Kati.

Rais wa Russia, Vladimir Putin aliwasili katika Mji Mkuu wa Kazakhstan wa Astana, jana asubuhi kuungana na viongozi wengine watakaohudhuria mkutano wa Shirika la Ushirikiano la Shanghai (SCO), ambalo ni kundi linaloongozwa na China na kujumuisha mataifa ya Asia ya Kati, India na Iran.

Kiongozi wa China, Xi Jinping aliwasili Kazakhstan juzi na viongozi hao wawili wataungana kwenye mkutano huo ambao wanautazama kama chombo muhimu cha kuendeleza malengo yao ya kimkakati katika kanda ya Ulaya na Asia.

Russia na China wamezidisha uhusiano wao wa kisiasa, kijeshi na kiuchumi tangu ilipoanza vita yake Ukraine. **DW**

# Serikali Kenya yalaani vurugu

**NAIROBI,** Kenya

SERIKALI ya Kenya imelaani vitendo vya vurugu vinavyofanywa na baadhi ya watu katika maandamano yanayoendelea nchini humo.

Juzi polisi walitumia mabomu ya machozi na maji ya kuwasha kujaribu kuwatawanya waandamanaji waliojitokeza mitaani wakitaka serikali ya Willium Ruto kujiuzulu.

Hata hivyo watu wachache walijitokeza katika maandamano hayo, tofauti na yale ya juma lililopita.

Hata hivyo yalikuwa ya vurugu na kusababisha polisi kulazimika kutumia nguvu kuwadhibiti baadhi ya raia waliojaribu kupora mali na kuharibu miundombinu.

Tayari waasisi wa maandamano hayo maarufu kama Gen Z kufikia kakati wao mpya kutokana na kushuhudia baadhi ya watu wakitumia nafasi hiyo kufanya vitendo vya kihalifu ikiwemo kupora maduka ya watu na kuchoma moto magari.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Kenya, Kithure Kindiki, alitoa tarifa kulaani vitendo vya kihalifu, akisema kuna watu wamepanga kufanya vurugu zaidi siku ya Alhamisi na Jumapili, na kwamba watashughulikiwa kikamilifu.

Vurugu zinazoshuhudiwa maeneo mengi ambako uporaji na uchomlaji moto wa mali umefanyika.

Maandamano hayo yameibua mjadala mtandaoni kuhusu uwezekano wa wahalifu waliokodiwa na wanasiasa kutumika kufanya vurugu ili kuondoa kile wadadisi wanasema uhalali wa maandamano ya amani.

Maandamano hayo yanafanyika licha ya serikali kukubali kuondoa muswada tata wa fedha uliokataliwa na raia.

Waandamanaji wamebadili uelekeo wa madai yao, sasa wanataka maofisa wanaotuhumiwa kwa rushwa kuondolewa kazini na Serikali kuondoka madarakani. **RFI**

# MANDONGA, MAUGO ULINGONI GEITA JULAI, KUTUNISHA TASAF

**Na Faustine Feliciane**

BONDIA mwenye ‚mbwembe', Karim Mandonga anatarajia kupigana na mkongwe, Mada Maugo katika pambano maalum litakalofanyika Julai 28, mwaka huu mkoani Geita.

Pambano hilo ni kwa ajili ya kukusanya fedha zitakazoingizwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kusaidia kulipia huduma ya Bima ya Afya kwa Kaya masikini katika mikoa ya Dodoma, Mbeya, Pwani na Geita.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Taasisi ya Lady in Red, waandaaji wa pambano hilo, Sophia Mwakagenda, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, alisema lengo lao ni kuwasaidia Watanzania wengine ambao wanashindwa kuwa na kadi ya bima ya afya.

Mwakagenda alisema pia kutakuwa na mapambano mengine yatakayosindikiza mabondia ambayo yatatangazwa baada ya kukamilika kwa mazungumzo.

"Kutakuwa pia na mapambano mengine ya hisani, kuna mapambano ya wabunge kwa wabunge pamoja na mabondia wengine wakubwa," alisema Mwakagenda.

Aliongeza wadau wengine wanatakiwa wawaunge mkono kwa kujitokeza katika mapambano hayo ili kufikia malengo ya kusaidia jamii hasa kwa kaya za watu wasiojiweza kwa kutumia sekta zao mbalimbali.

"Kuna Watanzania wengi wanahitaji msaada, watu wengine katika sekta nyingine watumie sekta zao kuchangisha fedha ili kusaidia jamii katika maeneo mengine yanayowazunguka," Mwakagenda alisema.

Mratibu huyo alitaja mabondia wengine mapambano watakaopanda ulingoni watakuwa ni Japhert Kaseba lakini pambano kubwa litawahusisha Ibra Classic dhidi ya bondia mwingine atakayetangazwa baadaye.

Kwa upande wa Mandonga amewataka watu wa Kanda ya Ziwa kujitokeza kwa wingi kushuhudia ngumi ya ‚mbeku' ikimchakaza Maugo.

"Nashukuru kupewa tena Maugo, pambano letu lililopita kule Morogoro aliniponyoka, sasa naenda kumalizana naye Geita, hatotoka salama," alitamba Mandonga.

Maugo aliwaomba watu wa Kanda ya Ziwa hususani kwao Mara kujitokeza kwa wingi kuona anavyompa kipigo cha pili mfululizo Mandonga.

"Mandonga ni mwongeaji tu, sasa anakuja kwenye ardhi yetu, wana Kanda ya Ziwa, ngumi nilizompiga Morogoro ni za kawaida, sasa naenda kummaliza kwetu," alisema Maugo.




Bondia Mada Maugo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu pambano lake dhidi ya Karim Mandonga (kushoto), litakalofanyika Julai 28, mwaka huu mkoani Geita. Kulia ni mratibu wa pambano hilo, Sophia Mwakagenda. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# TFF yawaita wadau Sabasaba

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), linawaomba wadau wa michezo nchini hususan soka kutembelea katika banda lao lililopo kwenye Maonyesho ya 48 Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ili kujifunza mambo mbalimbali kuhusiana na shirikisho hilo, imeelezwa.

Akizungumza jijini jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema wadau wa michezo wakifika hapo watapata kufahamu historia mbalimbali kuhusiana na mchezo huo lakini pia watapata elimu ya namna shirikisho linavyofanya kazi zake za kila siku.

Kidao alisema wadau watafahamu kanuni zinazosimamia uendeshaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kamati ya Saa 72 ambayo husikiliza na kupitia ripoti za mechi za Ligi Kuu, Ligi ya Championship, First League na mashindano mengine yaliyoko chini ya TFF.

Alisema pia wageni wote watakaofika kwenye banda la TFF watajulishwa muundo wa shirikisho hilo, Mkutano Mkuu na Kamati ya Utendaji inavyopatikana na inavyofanya kazi zake.

„Tunatoa pia nafasi kwa wadau wetu tunaofanya nao kazi, tunaoshirikiana nao, wito wangu ni wapenzi wa mpira wa mguu kujitokeza kujifunza, ni chombo kipi chenye mamlaka ya kutoa maamuzi, chombo kipi kinatoa maamuzi kuhusiana na mechi, chombo kipi kinatoa maamuzi," alisema Kidao.

Aliongeza mafanikio yote yanayoonekana katika shirikisho hilo yanatokana na namna mfumo wa uendeshaji uliopo na hii ni nafasi nafasi pekee wadau kufahamishwa mambo mbalimbali ambayo wanahitaji kupata ufafanuzi.

## New City kuacha 10, kuanza 'tizi' Julai 15

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kunusurika kushuka daraja na kuhakikisha inakuwa na kikosi imara, uongozi wa New City FC umesema utaanza maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar mapema.

New City imebakia katika Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16 kutoka Unguja na Pemba baada ya kupata ushindi katika mchezo wake wa mwisho.

Kocha Msaidizi wa New City, Razak Rajab, alisema kuelekea msimu mpya wa 2024/2025, wanatarajia kufanya usajili mzuri ambao utaendana na kasi ya ligi hiyo huku wakijipanga kuacha wachezaji 10.

Rajab alisema bado wanaendelea na mazungumzo na wachezaji ambao wanawahitaji na wanaamini wakifia makubaliano, watakuwa na kikosi imara na kitakachokabiliana na ushindani uliopo kwenye ligi hiyo.

"Tunatarajia kuanza mazoezi 'Pre Season' kuanzia Julai 15. Tunataka kuwa na maandalizi mazuri na muhimu sana ili kuhakikisha msimu huu mpya hatufanyi makosa, tunatarajia kuwa na msimu mpya wenye mafanikio makubwa," Rajab alisema.

## Makapu na wenzake watemwa Mashujaa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa imetangaza kuachana na wachezaji sita ambao waliichezea timu hiyo katika msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwamo mchezaji wa zamani wa Yanga, Said Makapu.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari ya klabu hiyo jana, haikutoa sababu halisi, badala yake ilisema hawatakuwa sehemu ya kikosi chao kuelekea msimu ujao wa 2024/2025.

Mbali na kiungo mkabaji, Makapu, nyota wengine walioachwa ni Samson Madeleke, Mchembe Maganda, Ally Ramadhani ‚Oviedo', Michael Masinda na Shadrack Ntabindi.

Hata hivyo, Mashujaa tayari imeshaondokewa na wachezaji wao nyota akiwamo straika wake tegemeo, Adam Adam, aliyejiunga na Azam FC, huku taarifa zikisema Omari Omari, wakati wowote anaweza kutambulishwa kutua Simba, huku Reliants Lusajo akiwa ananukia Dodoma Jiji.

Hata hivyo, taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema mabosi wanaendelea na usajili na ukikamilika watapanda boti kuelekea Zanzibar kuweka kambi ya maandalizi ya msimu mpya wakiwa chini ya Kocha Mkuu, Mohamed Abdallah ‚Bares.'

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CALAFIORI AWINDWA ENGLAND**
LIVERPOOL, Arsenal, Chelsea na West Ham zote zinavutiwa na beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, lakini watalazimika kulipa zaidi ya pauni milioni 40 ili kumnunua kutoka Bologna. (***Express***)

**WILLIAMS HAJASHAWISHI**
BAADHI ya wakurugenzi wa Barcelona bado hawajashawishika kuhusu ubora wa kumsajili winga nyota wa Hispania kwenye Euro 2024, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21, kutoka Athletic Bilbao.(***Sport***)

**HALL AIKACHA BRIGHTON**
KLABU ya Brighton imeachwa mdomo wazi baada ya Chelsea kukubali dili la kumsajili kiungo, Kiernan Dewsbury-Hall mwenye umri wa miaka 25, kutoka Leicester ingawa mchezaji huyo alikuwa amefanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Seagulls na ada ilikubaliwa kati ya klabu hizo mbili. (***Telegraph***)

**UNITED HAINA MPANGO NA ARAUJO**
KLABU ya Manchester United haina nia ya kutafuta dili la kumnunua mlinzi wa Barcelona, Ronald Araujo licha ya nia ya muda mrefu ya kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 25. (***Football Transfers***)

**GOLDING ANUKIA LEICESTER**
KLABU ya Leicester City inakaribia kufikia makubaliano ya kumnunua kiungo wa kati Michael Golding mwenye umri wa miaka 18 kutoka Chelsea. (***The Athletic***)

**VLACHODIMOS ATAKIWA**
NEWCASTLE United inajaribu kufanya mazungumzo ya kumsajili mlinda lango wa Nottingham Forest na Ugiriki, Odysseas Vlachodimos mwenye umri wa miaka 30, kama sehemu ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Scotland, Elliot Anderson mwenye miaka 21, kwenda City Ground. (***Daily Mail***)

**NEWCASTLE KUTOMUUZA ISAAK**
KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe ameweka wazi katika mazungumzo na bodi ya klabu hiyo kwamba hawatakiwi kumuuza mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isaak mwenye miaka 24 msimu huu huku kukiwa na nia kutoka kwa Chelsea. (***Fabrizio Romano***)


**DORTMUND YAMTAKA GRAY**
KLABU ya Borussia Dortmund inavutiwa na kiungo wa kati wa Leeds United, Archie Gray mwenye umri wa miaka 18. (***Bild***)

**DAVID ANYATIWA**
KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David mwenye miaka 24, ambaye pia anahusishwa kutaka kuhamia kwenye klabuya Chelsea. (***Football Insider***)

**KUDUS AHUSISHWA KUONDOKA W'HAM**
MCHEZAJI wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye miaka 23, amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka West Ham lakini klabu hiyo bado haijapokea ofa ya kiungo huyo mshambuliaji. (***Sky Germany***)

**NAPOLI KUMPIGA BEI OSIMHEN**
KLABU ya Napoli itazingatia ofa ya kiwango cha euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye miaka 25, na mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku anayetarajiwa kuchukua nafasi yake. (***Calciomercato***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ETO'O AKALIWA KOONI CAMEROON

## ●●● Muungano wa klabu za soka nchini humo wanadai kiongozi huyo ana....

**YOAUNDE,** Cameroon

MUUNGANO wa klabu za soka nchini Cameroon (AFCA) umemtaka Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini humo, Samuel Eto'o kujiuzulu kwa kinachodaiwa kubaini kuwa ana hati ya uraia pacha.

AFCA wanadai kiongozi huyo mkuu wa FECAFOOT ana uraia wa Cameroon na Hispania, hivyo anakosa sifa za kuendelea kukalia kiti hicho.

Marais zaidi ya 50 wa klabu nchini humo, wameiandikia barua Kamati ya nidhamu ya Shirikisho la soka nchini humo (FECAFOOT) kumuamuru Eto'o abwage manyanga.

**Disemba 2021, Eto'o aliibuka kidedea katika kinyang'anyiro cha kutwaa kiti hicho ambacho inaelezwa kilikuwa na madudu mengi yaliyosababisha mgawanyiko katika soka la miamba hao wa soka barani Afrika.**

Hata hivyo, katika miaka yake miwili uongozini amekumbwa na mizozo kadhaa ikiwemo dhidi ya Waziri wa Michezo na Elimu, Narcisse Kombi kwa kilichoelezwa kuingiliwa mamlaka yake ya urais wa FECAFOOT.

Kumekuwa na fikra mseto juu ya uwezo wa kuongoza kwa mfumania nyavu huyo wa zamani wa Chelsea, Real Madrid na Barcelona ambaye wengine wakiamini ni mponyaji Ila wengine wakisema ni mwenye majivuno.

# BARCELONA KUMUUZA KOUNDE ARSENAL




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wanafikiria kumuuza Jules Kounde huku klabu ya Arsenal ikionyesha nia ya kumtaka, lakini watasubiri hadi mustakabali wa Ronald Araujo uamuliwe kabla ya kufanya uhamisho wao mwingine, kulingana na ripoti.

Miamba hao wa Katalunya huenda wakalazimika kusikiliza ofa kwa wachezaji wengi wa kikosi chao msimu huu wa majira ya joto ili kupambana na matatizo yao ya kifedha.

Hata hivyo wamemuongeza Kounde kwenye orodha ya wachezaji ambao wako tayari kuwaondoa.

Beki huyo mahiri tayari amevutia macho ya timu kufikia sasa katika kipindi hiki cha uhamisho, huku Arsenal ya Mikel Arteta ikiwa moja ya klabu zinazomtaka.

Sasa, kulingana na ripoti kutoka Sport inaonekana Barca wapo tayari kumuuza Kounde kwa Arsenal, lakini ikiwa tu Araujo, ambaye amekuwa akihusishwa sana kuondoka, atasalia katika klabu hiyo.

Barcelona wanatarajia ada ya si chini ya euro milioni 60 kwa Kounde na ‚itafungua mazungumzo' na Washikabunduki hao, ambao wameanzisha harakati za kumtaka.

Kuhama kwa Kounde kutapunguza mzigo mkubwa kwenye bili ya mishahara ya Barcelona.

Ingawa Barca wanaitaka Arsenal kuwa na subira kuhusu uamuzi wa Kounde.

Nyota huyo ambaye kwa sasa yuko kwenye michuano ya Euro 2024 akiwa na Ufaransa, aliichezea Barca mechi 48 msimu wa 2023/24, akifunga mabao mawili na kusaidia kupatikana mabao manne.

# Alvarez ajumuishwa Argentina ya Olimpiki



**BUENOS AIRES,** Argentina

KOCHA Javier Mascherano aliwajumuisha washindi wanne wa Kombe la Dunia katika kikosi alichotangaza Jumanne cha Argentina kitakachoshiriki Michezo ya Olimpiki huko Paris baadaye msimu huu wa majira ya joto.

Mshambuliaji wa Manchester City, Julian Álvarez na beki mkongwe wa Benfica, Nicolás Otamendi walikuwa miongoni mwa majina hayo.

Kama ilivyotarajiwa, Lionel Messi si sehemu ya kikosi hicho baada ya nyota huyo wa Inter Miami kuwahi kusema kucheza kwenye Olimpiki itakuwa ngumu katika msimu wa majira ya joto ambao tayari una shughuli nyingi.

Messi, ambaye amekuwa na majeraha mwaka huu, sasa anacheza Copa América pamoja na Álvarez na Otamendi, akilenga kutetea taji la Bara hilo ambalo timu hiyo ilishinda mwaka 2021.

Ushindi huo ulikuwa chachu kwa Argentina kunyanyua Kombe la Dunia mwaka wa 2022.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 37 alishinda medali ya dhahabu ya Olimpiki huko Beijing mwaka 2008.

Mascherano, ambaye alishinda medali ya dhahabu ya Olimpiki kama mchezaji mwaka wa 2004 na ‚08, atawaongeza kipa Gerónimo Rulli, Otamendi na Álvarez kwenye kikosi chake baada ya Copa América kukamilika.

Kiungo Claudio Echeverri, aliyesajiliwa hivi majuzi na Manchester City kutoka River Plate, pia atakuwa sehemu ya kikosi hicho..

Argentina itacheza mechi mbili za kirafiki nchini Ufaransa kabla ya mechi yao ya ufunguzi ya michuano ya Olimpiki dhidi ya Morocco Julai 24.

Timu hiyo ipo kwenye kundi B pamoja na timu za Morocco, Iraq na Ukraine.

# Colombia waivimbia Brazil

**CALIFORNIA,** Marekani

BRAZIL ilitoka sare ya 1-1 na Colombia siku ya Jumanne mjini Santa Clara, California na kufuzu kwa robo fainali ya Copa América.

Colombia, waliomaliza kileleni mwa Kundi D wakiwa na pointi saba, watamenyana na Panama katika robo fainali huku Brazil walio nafasi ya pili watachuana na washindi wa Kundi C, Uruguay.

Dakika 15 za kwanza kwenye Uwanja wa Levi's ziliifanya Colombia kuwa nyuma baada ya Raphinha kupiga shuti kali na kuwapa Brazil bao la kuongoza dakika ya 12.

Colombia walipata bao la Davinson Sanchez lililokataliwa kwa sababu ya kuotea kabla ya Daniel Munoz kusawazisha dakika za majeruhi katika kipindi cha kwanza.

„Ilikuwa mechi ambayo sote tulitaka kucheza ili kujipima katika wakati mzuri kwa timu. Nadhani tumepiga hatua nyingine mbele leo," alisema kocha wa Colombia Nestor Lorenzo.

„Ukiwa na Brazil huwezi kupuuza timu hata kwa sekunde moja. Hisia ni moja ya kuridhika dhidi ya mpinzani mgumu na sasa tutafikiria kuhusu Panama," alisema kocha huyo.

Kabla ya bao la kusawazisha, Brazil walidhani walipata penalti dakika ya 42 wakati Munoz alipomwangusha Vinicius Junior kwenye eneo la hatari, lakini picha za marudio za televisheni zilionekana kuonesha beki wa Colombia aligusa mpira.

Licha ya joto kali la California, hakuna upande ulioruhusu nguvu kushuka baada ya mapumziko.

Raphinha alipiga mkwaju wa faulo nje kidogo, na Andreas Pereira akamjaribu Camilo Vargas kwa juhudi za masafa marefu, lakini Colombia walishikilia sare na kurefusha mbio zao za kutopoteza na kufikia mechi 26.

Vinícius Júnior alipata kadi ya njano katika dakika ya saba ambayo itamfanya kukosa mechi ya robo fainali dhidi ya Uruguay.

Wachezaji walionyesha kandanda safi la kuburudisha katika fainali ya Kundi D, huku Mbrazil Bruno Guimarães akiita Colombia „jiwe katika kiatu chetu" kabla ya Jumanne.

Kile ambacho kilitarajiwa kuwa mechi kali, ya kimwili na iliyojaa faulo zaidi ya kukidhi mshangao huo wa kadi tano za njano.

Umati wa watu 70,971 ulihudhuria mchezo huo na michezo 24 ya hatua ya makundi ilivuta watu 1,115,400 kwa wastani wa watu 46,475.

„Tunapaswa kuwa waaminifu kwetu, bado tuna mengi ya kukua, mengi ya kuboresha, haswa katika michezo hii mikubwa," alisema beki wa Brazil, Marquinhos.

## Chama: 'Thank you' Simba SC

INATOKA UK. 24

idara ili kurejesha heshima na furaha kwa mashabiki na wanachama wa Wekundu wa Msimbazi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema bado hawajamaliza mchakato wa kusajili wachezaji wapya.

"Familia inazidi kuongezeka, napenda kuwaambia kila mchezaji ambaye tutamtangaza ni mchezaji mwenye rekodi, anayekuja kutupeleka katika malengo yetu, tutakuwa moto, tumejenga kikosi imara," Kajula aliongeza.

Juzi Simba ilitangaza kukamilisha usajili wa Joshua Mutale kutoka Zambia na Steven Mukwala, ambaye ni nyota wa Timu ya Taifa ya Uganda (Uganda Cranes), aliyekuwa akiitumikia Asante Kotoko ya Ghana.

Hata hivyo bado Simba bado haijatangaza kocha mkuu mpya ambaye anakuja kurithi mikoba iliyoachwa na Mwarabu wa Algeria, Abdelhak Benchikha.

## Diarra, Mustafa wabakia Tanzania

INATOKA UK. 24

kimataifa.

"Tunataka msimu ujao kufanya vizuri zaidi, kuanzia katika mashindano ya ndani na Klabu Bingwa Afrika, tunataka tufike mbali zaidi ya msimu huu ulioisha," alisema Kamwe.

Aliongeza Diarra amekuwa na mchango mkubwa katika kikosi cha timu hiyo na amechangia mafanikio waliyoyapata katika kipindi chote tangu ajiunge na mabingwa hao.

"Lengo letu ni kuona tunafanya vizuri zaidi ya msimu uliopita katika mashindano yote, kwa hiyo uongozi hautamwacha mchezaji tunayemhitaji aondoke kwenye kikosi," Kamwe alisema.

Wakati huo huo, Azam FC, imempa mkataba wa miaka miwili golikipa wake namba moja, Muhamad Mustafa, ambaye ni raia wa Sudan.



"Muhamad bado yupo hapa," ilisema taarifa rasmi iliyoandikwa na klabu hiyo ya Chamazi.

Mustafa, ambaye ni kipa chaguo la kwanza wa Timu ya Taifa ya Sudan, alikuwa akiitumikia Azam kwa mkataba wa mkopo akitokea El Mereikh.

# AUSSEMS AITABIRIA MAZURI SINGIDA BS LIGI KUU BARA

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya kuwasili nchini na kusaini mkataba wa kuifundisha Singida Black Stars, Kocha Mkuu, Patrick Aussems, amesema timu hiyo itakuwa miongoni mwa timu zinazocheza soka safi la kuvutia.

Aussems, kocha wa zamani wa Simba, amesema hawezi kuahidi kikosi hicho kitachukua ubingwa lakini anaamini baada ya miaka michache Singida Black Stars itakuwa klabu bora hapa Tanzania.

"Nilikuwa na hapa nikiifundisha Simba, tulijenga timu na kuanza kufanya vizuri na kuwa na jina kubwa, naamini na Singida itakuwa hivyo hivyo," alisema Aussems.

Aliongeza anatarajia kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wa klabu pamoja na wachezaji.

"Nje ya Tanzania inajulikana zaidi klabu ya Simba na Yanga kidogo, hii ni nafasi ya kuiandaa Singida ili kuwa miongoni mwa timu bora hapa Tanzania, hilo linawezekana kwa ushirikiano wa watu wote, benchi la ufundi, wachezaji na viongozi," alisema Aussems.

Kocha huyo alisema anajua Ligi Kuu Tanzania Bara imekuwa na ushindani na hiyo inasaidia kukuza soka la hapa nchini.

"Nimejiandaa kukabiliana na ushindani kutoka kwa kila timu inayoshiriki Ligi Kuu, hakuna mechi rahisi, hakuna tena timu ndogo," Aussems alisema.

Wakati huo huo mabosi wa timu hiyo wameomba kushiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame yanayotarajiwa kufanyika hapa nchini hivi karibuni.



Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao (kulia), akisikiliza maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Masoko wa shirikisho hilo, Aaron Nyanda, katika banda la TFF lililopo katika Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: TFF**

# Coastal, JKU kundi moja michuano Kagame CUP

**Na Shufaa Lyimo**

COASTAL Union ya Tanga na JKU kutoka Zanzibar zimepangwa Kundi A katika mashindano ya Kombe la Kagame yatakayofanyika kuanzia Julai 9 hadi 21, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akiongoza droo hiyo, Meneja Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema michuano hiyo imepangwa katika makundi matatu ambapo Kundi A litaundwa na Coastal Union (Tanzania), Ali Wadi FC (Sudan), JKU (Zanzibar) na Dekedaha FC kutoka Somalia.

Kizuguto alisema Al Hilal ya Sudan, Gor Mahia FC (Kenya), Red Arrows FC (Zambia) na Telkom FC (Djibouti) zenyewe ziko katika Kundi B wakati Kundi C linajumuisha SC Villa (Uganda), APR (Rwanda), Singida Black Stars (Tanzania) na El Merriekh Bantui (Sudani Kusini).

Meneja huyo alisema mechi za mchana zitachezwa kwenye Uwanja mpya wa KMC uliopo Mwenge na zile za usiku zitafanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex.

"Kila timu itacheza michezo mitatu hakutakuwa na michezo ya robo fainali, kwa zile ambazo zitafanya vyema, moja kwa moja zitaingia hatua ya nusu fainali," alisema meneja huyo.

Aliongeza maandalizi yanaendelea vizuri na wanaamini mashindano hayo yatasaidia timu za CECAFA kujiandaa na msimu mpya wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.



# Michezo

Alhamisi Julai 4, 2024

Nipashe




Eto'o akaliwa kooni Cameroon

UK. 21

# Chama: 'Thank you' Simba SC

## ●●● Kiungo huyo Mzambia afunguka hakuna atakayebadilisha historia...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI ikiendelea kushusha vifaa vipya kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake, aliyekuwa kiungo wa kimataifa wa Simba kutoka Zambia, Clatous Chama 'Mwamba', rasmi amewaaga mashabiki na wanachama wa Wekundu wa Msimbazi huku akisema historia haitabadilika.

**Yanga ilitangaza kumsajili Chama mapema wiki hii ikiwa ni baada ya mkataba wa Simba na Mzambia huyo kumalizika Juni 30, mwaka huu.**

Nyota huyo jana aliandika pia katika ukurasa wake wa Instagram yeye ni mchezaji wa Yanga na Timu ya Taifa ya Zambia maarufu Chipolopolo.

Chama ambaye alijiunga na Simba akitokea Lusaka Dynamo FC ya Zambia alisema jana alikuwa na miaka sita yenye furaha, mafanikio na changamoto mbalimbali.

Kiungo huyo aliyetua Simba mwaka 2018, halafu miaka mitatu aliuzwa katika klabu ya RS Berkane ya Morocco na baadaye kurejea kwa Wekundu wa Msimbazi alisema alifanya kazi yake Simba kwa upendo na alipata heshima kutoka kwa wachezaji, viongozi na mashabiki.

"Miaka sita iliyopita nilikuja kama mgeni. Mlinipa malengo na changamoto za kunifanya kuwa bora zaidi. Sina la ziada zaidi ya heshima kwa kila mmoja wenu kwa upendo na ushirikiano mlionipa kwa miaka yote, hakuna anayeweza kubadilisha historia tuliyoitengeneza pamoja.

Nawatakia kila la kheri na tuendelee kuonana katika nyakati nzuri," alimaliza Chama ambaye ana umri wa miaka 33.

Hata hivyo Chama ambaye ni mmoja wa wachezaji nyota katika kikosi cha Chipolipolo, utambulisho wake wa kujiunga na Yanga haujafanana na thamani aliyonayo.

Simba ilifikia uamuzi wa kutompa kiasi cha fedha ambazo alikihitaji kwa kuzingatia umri na kiwango alichokionyesha katika mwaka wake wa mwisho wa mkataba.

Ubora wa Chama ambaye amezaliwa kwenye familia ya wanasoka ulianza kuonekana alipokuwa akiitumikia ZESCO United ya Zambia ambapo mwaka 2016 alionyesha kiwango cha juu na kusajiliwa na Al Ittihad ya Misri mwaka 2017 ingawa alicheza kwa muda mfupi na kurejea kwao Zambia.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili mabosi wa klabu hiyo wanaendelea kufanya usajili bora ambao utawafikisha katika malengo yao kwenye mashindano yote watakayoshiriki msimu ujao.

Ahmed alisema wamefahamu walipokosea na sasa wanajiimarisha katika kila

INAENDELEA UK. 23



Chama

## Diarra, Mustafa wabakia Tanzania

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Yanga umefanikiwa kumbakisha kipa wake chaguo la kwanza, Djugui Diarra, kwa kumpa mkataba wa miaka miwili ya kuendelea kuwatumikia mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Diarra, ambaye ni golikipa chaguo la kwanza la Timu ya Taifa ya Mali, amesaini mkataba utakaomweka klabuni hapo hadi mwaka 2026.

Baada ya majadiliano na uongozi wa Yanga kufikia pazuri, Diarra amekubali kuendelea kuitumikia timu hiyo huku akizifungia ‚macho' ofa kutoka katika klabu nyingine zilizokuwa zinataka huduma yake.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jijini Dar es Salaam jana uongozi wao uko makini katika mchakato wa usajili wa wachezaji kwa kuhakikisha inawabakisha nyota wote inaowahitaji.

Kamwe alisema chini ya Rais Hersi Said, Yanga imedhamiria kuona timu yao inaendelea kufanya vizuri katika msimu mpya wa mashindano ya ndani na ya

HABARI UK. 23




9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042